


# Tangazo la Kulinda Haki za Watoto Wenye Ulemavu na Wazazi Wao

## Sheria ya Elimu kwa Watu Wenye Ulemavu

Kitengo cha Watu Maalum na Msaada wa Wanafunzi | Februari 2024

# Utangulizi

Sheria ya Elimu kwa Watu Wenye Ulemavu (IDEA), sheria ya serikali kuu inayohusu elimu ya wanafunzi wenye ulemavu, inazitaka shule kumpatia wazazi wa mtoto wenye ulemavu tangazo lenye maelezo kamili ya kulinda haki za watoto wenye ulemavu na wazazi wao kwa mujibu wa IDEA, kanuni za Wizara ya Elimu ya Marekani, na sheria na kanuni za Tennessee.

Nakala ya tangazo hili lazima wapewe wazazi mara moja tu kwa mwaka wa shule, isipokuwa kama nakala hiyo lazima wapewe wazazi katika matukio yafuatayo:

1. Rufaa ya awali au ombi la mzazi kwa ajili ya tathmini
2. Kupokea malalamiko ya kwanza ya Jimbo kwa mujibu wa 34 C.F.R. 300.151 hadi 300.153 §§ katika mwaka wa shule
3. Kupokea malalamiko ya kwanza ya mchakato unaostahili kwa mujibu wa § 300.507 katika mwaka wa shule
4. Hatua ya kinidhamu ambayo inajumuisha kubadilishiwa darasa
5. Ombi la mzazi [34 C.F.R. § 300.504(a)]

Tangazo hili la kulinda haki za watoto wenye ulemavu na wazazi wao ni pamoja na maelezo kamili ya kulinda haki za watoto wenye ulemavu na wazazi wao kwa mujibu wa § 300.148 (upangaji unaohusu upande mmoja katika shule binafsi kwa gharama ya serikali), §§ 300.151 hadi 300.153 (taratibu za malalamiko za jimbo), § 300.300 (idhini), §§ 300.502 hadi 300.503, §§ 300.505 hadi 300.518, na §§ 300.530 hadi 300.536 (kulinda haki za watoto wenye ulemavu na wazazi wao katika Sehemu ndogo E ya Sehemu B ya kanuni), na §§ 300.610 hadi 300.625 (usiri wa utoaji taarifa katika Sehemu ndogo F).

Taarifa zaidi kuhusu mada zilizo katika tangazo hili zinaweza kupatikana katika tovuti ya idara: https://www.tn.gov/education/legal-services/special-education-legal-services.html.

# YALIYOMO


## Maelezo ya Jumla 5

*Taarifa Iliyoandikwa Kabla* 5
*Lugha ya Mama* 6
*Barua za Kielektroniki* 6
*Idhini ya Wazazi - Fasili* 6
*Idhini ya Wazazi* 6
*Wakati Gani Mipango ya Elimu ya Iliyopambanuliwa (IEPs) Itaanza Kutumika* 9
*Tathmini Huru za Elimu* 9

## Usiri wa Taarifa 11

*Tangazo kwa Wazazi* 11
*Taarifa ya Upatikanaji* 12
*Taarifa Kuhusu Mtoto Zaidi ya Mmoja* 13
*Orodha ya Aina na Sehemu za Taarifa* 13
*Ada* 13
*Marekebisho ya Taarifa kwa Ombi la Mzazi* 13
*Fursa ya Usikilizaji Shauri* 13
*Taratibu za Usikilizaji Shauri* 14
*Majibu ya Shauri* 14
*Idhini ya Kutoa Taarifa Zinazoweza Kumtambulisha Mtu* 14
*Ulinzi* 15
*Uharibifu wa Taarifa* 15

## Taratibu za Malalamiko ya Jimbo na Utatuzi wa Mizozo 15

*Tofauti kati ya Taratibu za Malalamiko Yanayostahili Kusikizwa na za Malalamiko ya Kiutawala* 15
*Taratibu za Malalamiko ya Kiutawala* 16
*Muwasilisha Malalamiko* 17
*Fomu za Mfano* 18
*Upatanishi* 18
*Fomu za Mfano* 19
*Taratibu za Malalamiko Yanayostahili* 19
*Kuwasilisha Malamiko Yanayostahili* 19
*Malalamiko Yanayostahili* 20
*Fomu za Mfano* 21
*Mchakato wa Upatanisho* 22
*Usikilizaji wa Shauri Unaostahili* 24
*Haki za Usikilizaji wa Shauri* 25
*Maamuzi ya Shauri* 25
*Rufaa* 26

*Ratiba ya matukio* 26
*Hatua za Kiraia* 27
*Ada ya Mwanasheria* 27

**Taratibu za Kuwaadhibu Watoto Wenye Ulemavu** **29**

*Mamlaka ya Wafanyakazi wa Shule* 29
*Mabadiliko ya Darasa kwa Sababu za Kinidhamu* 32
*Kupangwa Darasa Wakati wa Rufaa* 33
*Ulinzi kwa Watoto Ambao Bado Hawastahiki Kupata Elimu Maalum na Huduma Zinazohusiana Nayo* 34
*Rufaa na Hatua za Chombo cha Utekelezaji wa Sheria na Mamlaka za Mahakama* 35

**Masharti ya Upangaji wa Upande Mmoja Unaofanywa na Wazazi wa Watoto katika Shule Binafsi kwa Gharama za Serikali** **35**

**Fomu ya Malalamiko ya Kiutawala** **37**

**Fomu ya Maombi ya Upatanisho** **38**

**Fomu ya Maombi ya Usikilizaji wa Shauri Unaoshahili** **39**

**Huduma za Utetezi** **40**

**Huduma za Sheria za Bule na za Gharama Nafuu** **40**

# Maelezo ya Jumla

## *Taarifa Iliyoandikwa Kabla*

*34 C.F.R. § 300.503 na Bodi ya Elimu ya Jimbo (SBE) Rule § 0520-01-09-.15(4)*

### Tangazo

Wilaya ya shule yako lazima ikupe taarifa fulani kwa maandishi, angalau siku 10 za shule kabla ya:

1. kupendekeza kuanzisha au kubadilisha kitambulisho, tathmini, au nafasi ya kielimu ya mtoto wako, au utoaji wa Elimu ya Umma Inayofaa Bila Malipo (FAPE) kwa mtoto wako; **au**
2. kukataa kuanzisha au kubadilisha kitambulisho, tathmini, au nafasi ya kielimu ya mtoto wako au utoaji wa FAPE kwa mtoto wako.

### Maudhui ya tangazo

Tangazo la maandishi lazima:

1. lifafanue hatua ambayo wilaya ya shule yako inapendekeza au inakataa kuchukua;
2. lielezee kwa nini wilaya ya shule yako inapendekeza au inakataa kuchukua hatua hiyo;
3. lifafanue kila utaratibu wa tathmini, uchunguzi, rekodi, au uripoti ambayo wilaya ya shule yako ilitumia katika kuamua kupendekeza au kukataa hatua hiyo;
4. lijumuisha maelezo kwamba una ulinzi kwa mujibu wa kanuni za kulinda haki za watoto wenye ulemavu na wazazi wao katika Sehemu B ya IDEA;
5. likwambie jinsi unavyoweza kupata maelezo ya kulinda haki za watoto wenye ulemavu na wazazi wao ikiwa hatua ambayo wilaya ya shule yako inapendekeza au inakataa sio rufaa ya awali ya tathmini;
6. lijumuishe nyenzo za kuwasiliana ili kusaidia kuelewa Sehemu B ya IDEA;
7. lifafanue machaguo mengine yoyote ambayo timu ya Mpango wa Elimu Iliopambanuliwa (IEP) ilizingatia na sababu kwa nini machaguo hayo yalikataliwa; **na**
8. litoe maelezo ya sababu zingine kwa nini wilaya ya shule yako ilipendekeza au ilikataa hatua hiyo.

### Tangazo katika lugha inayoeleweka

Tangazo lazima liwe:

1. limeandikwa katika lugha inayoeleweka kwa watu wote; **na**
2. limetolewa katika lugha mama yako au njia nyingine ya mawasiliano unayotumia, isipokuwa kama ni dhahiri haiwezekani kufanya hivyo.

Ikiwa lugha mama yako au njia nyingine ya mawasiliano si lugha inayoandikwa, wilaya ya shule yako lazima ihakikishe kwamba:

1. tangazo linatafsiriwa kwa mdomo kwa njia zingine katika lugha mama yako au njia nyingine ya mawasiliano;
2. unaelewa maudhui ya tangazo; **na**
3. pale ambapo ushahidi 1 na 2 wa maandishi umefikiwa.

## *Lugha ya Mama*

*34 C.F.R. § 300.29*

*Lugha mama,* inapotumika na mtu ambaye ambaye hazungumzi Kiingereza kwa ufasaha sana, inamaanisha yafuatayo:

1. Lugha hiyo kwa kawaida hutumiwa na mtu, au, kwa upande wa mtoto, lugha hiyo kwa kawaida hutumiwa na wazazi wa mtoto.
2. Katika mawasiliano ya moja kwa na (ikiwemo kufanya tathmini ya mtoto), lugha hiyo kwa kawaida hutumiwa na mtoto nyumbani au katika mazingira ya kujifunzia.

Kwa mtu mwenye uziwi, upofu, au asiye na lugha ya maandishi, njia ya mawasiliano ndiyo ambayo mtu huyo hutumia kwa kawaida (kama vile lugha ya ishara, Braille, au mawasiliano ya mdomo).

## *Barua za Kielektroniki*

*34 C.F.R. § 300.505*

Ikiwa wilaya ya shule yako inawapa wazazi chaguo la kupokea hati kwa barua pepe, unaweza kuchagua kupokea yafuatayo kwa barua pepe:

1. Taarifa iliyoandikwa kabla
2. Tangazo la kulinda haki za watoto wenye ulemavu na wazazi wao
3. Matangazo yanayohusu malalamiko yanayostahili

## *Idhini ya Wazazi - Fasili*

*34 C.F.R. § 300.9 na SBE Rule 0520-01-09-.03*

### Idhini

*Idhini* ina maana ifuatayo:

1. Umefahamishwa kikamilifu katika lugha mama yako au njia nyingine ya mawasiliano (kama vile lugha ya ishara, Braille, au mawasiliano ya mdomo) kuhusu taarifa zote zinazohusu hatua ambayo unaidhinisha.
2. Unaelewa na kukubalia kwa maandishi kwa hatua hiyo, na idhini inaielezea hatua hiyo na kuorodhesha rekodi (kama zipo) ambazo zitatolewa na kwa nani.
3. Unaelewa kuwa idhini ni ya hiari kwa upande wako na unaweza kuondoa idhini yako wakati wowote. Kuondoa idhini lazima kuwe kwa maandishi.

Kuondoa kwako idhini hakutangui kitendo ambacho kimetokea baada ya kutoa idhini yako na kabla ya kuiondoa.

## *Idhini ya Wazazi*

*34 C.F.R. § 300.300*

### Idhini ya tathmini ya awali

Wilaya ya shule yako haiwezi kufanya tathmini ya awali ya mtoto wako ili kubaini kama mtoto wako anastahiki kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA kupata elimu maalum na huduma zinazohusiana nayo bila kukupa taarifa ya maandishi ya hatua inayopendekezwa na bila kupata idhini yako kama ilivyoelezwa chini ya kichwa cha habari ***Idhini ya Mzazi.***

Wilaya ya shule yako lazima ifanye juhudi zinazofaa ili kupata idhini yako ya kujulishwa kwa ajili ya tathmini ya awali ili kuamua kama mtoto wako ni mtoto mwenye ulemavu.

Idhini yako ya tathmini ya awali **haimaanishi** kuwa umetoa idhini yako kwa wilaya ya shule kuanza kutoa elimu maalum na huduma zinazohusiana nayo kwa mtoto wako.

Ikiwa mtoto wako ameandikishwa katika shule ya serikali au unatafuta kumwandikisha mtoto wako katika shule ya serikali na umekataa kutoa idhini au umeshindwa kujibu ombi la kutoa idhini ya tathmini ya awali, wilaya ya shule yako inaweza, lakini haipaswi kuhangaika kufanya tathmini ya awali ya mtoto wako kwa kutumia upatanishi wa IDEA's au malalamiko yanayostahili, mkutano wa utatuzi, na taratibu za usikilizaji shauri linalostahili bila upendeleo. Wilaya ya shule yako haitakiuka majukumu yake ya kupata, kutambua na kutathmini mtoto wako ikiwa haitafuatilia tathmini ya mtoto wako katika hali hizi.

### Sheria maalum za tathmini ya awali ya watoto wanaolelewa na shirika la kulelea watoto la jimbo

Ikiwa mtoto ni mtoto wa kambo na haishi na mzazi wake, wilaya ya shule haihitaji idhini kutoka kwa mzazi kwa ajili ya tathmini ya awali ili kubaini kama mtoto ni mtoto mwenye ulemavu ikiwa:

1. licha ya jitihada zinazofaa za kufanya hivyo, wilaya ya shule haiwezi kumpata mzazi wa mtoto;
2. haki za wazazi zimekatishwa kwa mujibu wa sheria ya jimbo; **au**
3. hakimu ametoa haki ya kufanya maamuzi ya kielimu na kuridhia tathmini ya awali kwa mtu mwingine ambaye si mzazi.

*Mtoto wa Kambo*, kama ilivyotumika katika IDEA, inamaanisha mtoto ambaye ni:

1. mtoto wa kambo;
2. anachukuliwa kama mtoto wa kambo kwa mujibu wa sheria ya jimbo; **au**
3. katika malezi ya shirika la serikali la malezi ya watoto.

### Idhini ya mzazi kwa ajili ya huduma

Wilaya ya shule yako lazima ipate idhini yako kabla ya kutoa elimu maalum na huduma zinazohusiana nayo kwa mtoto wako kwa mara ya kwanza na lazima ifanye juhudi zinazofaa kufanya hivyo.

Ikiwa hutajibu ombi la kutoa idhini yako ili mtoto wako apate elimu maalum na huduma zinazohusiana nayo kwa mara ya kwanza, au ukikataa kutoa idhini hiyo, wilaya ya shule yako haiwezi kutumia ulinzi wa haki ya mtoto mwenye ulemavu na wazazi wake (yaani, upatanishi, malalamiko yanayostahili, mkutano wa utatuzi, au usikilizaji wa shauri bila upendeleo) ili kupata makubaliano au uamuzi kwamba elimu maalum na huduma zinazohusiana nayo (zinazopendekezwa na timu ya IEP ya mtoto wako) zinaweza kutolewa kwa mtoto wako bila idhini yako.

Ukikataa kutoa idhini yako ili mtoto wako apate elimu maalum na huduma zinazohusiana nayo kwa mara ya kwanza, au ikiwa hujibu ombi la kutoa idhini hiyo na wilaya ya shule haimpi mtoto wako elimu maalum na huduma ambazo iliomba idhini yako, wilaya ya shule yako:

1. haikiuki masharti ya kutoa Elimu ya Umma Inayofaa Bila Malipo (FAPE) kwa mtoto wako kwa kushindwa kwake kutoa huduma hizo kwa mtoto wako; **na**
2. haipaswi kuwa na mkutano wa Mpango wa Elimu Iliopambanuliwa (IEP) au kuandaa IEP ya mtoto wako kwa ajili ya elimu maalum na huduma zinazohusiana nayo na ambazo ziliombewa idhini.

Sheria hiyo hiyo inatumika ikiwa, baada ya utoaji wa awali wa elimu maalum na huduma zinazohusiana nayo, unaondoa idhini hiyo kwa maandishi na wilaya ya shule yako inatoa taarifa ya maandishi kabla ya kusitisha huduma. Ukiondoa idhini kwa maandishi baada ya utoaji wa huduma wa awali, wilaya ya shule yako haipaswi kurekebisha taarifa za elimu ya mtoto wako ili kuondoa marejeleo yoyote ya kupata elimu maalum kwa mtoto na huduma zinazohusiana nayo kwa sababu ya kuondoa idhini.

### Idhini ya mzazi kwa ajili ya kufanya upya tathmini

Wilaya ya shule yako lazima ipate idhini yako kabla ya kumtathmini upya mtoto wako, isipokuwa kama wilaya ya shule yako inaweza kuonyesha kwamba:

1. ilichukua hatua zinazofaa kupata idhini yako ya kumtathmini upya mtoto wako; **na**
2. hukujibu.

Ukikataa kutoa idhini ya mtoto wako kutathminiwa upya, wilaya ya shule inaweza lakini haipaswi, kumtathmini upya mtoto wako kwa kutumia upatanishi, malalamiko yanayostahili, mkutano wa utatuzi, na taratibu za usikilizaji shauri linalostahili ili kutaka kubatilisha kukataa kwako kutoa idhini ya kutathminiwa upya mtoto wako. Kama ilivyo katika tathmini za awali, wilaya ya shule yako haikiuki wajibu wake kwa mujibu wa  Sehemu B ya IDEA ikiwa itakataa kufanya upya tathmini kwa njia hii.

### Uhifadhi wa juhudi zinazofaa kupata idhini ya mzazi

Shule yako lazima ihifadhi hati za juhudi zinazofaa ili kupata idhini ya wazazi kwaaji ajili ya tathmini za awali, kutoa elimu maalum na huduma zinazohusiana nayo kwa mara ya kwanza, kwa ajili ya kufanya tathmini upya na kuwatafuta walezi wa mtoto kwa ajili ya kufanya tathmini za awali. Hati lazima zijumuishe taarifa ya majaribio ya wilaya ya shule katika maeneo haya, kama vile:

1. taarifa ya kina ya miito ya simu iliyofanyika au iliyojaribiwa na majibu ya kupiga huko simu;
2. nakala za barua zilizotumwa kwa wazazi na majibu yoyote yaliyopokelewa; **na**
3. taarifa za kina za zilizofanywa kwenda nyumbani kwa mzazi au anakofanyia kazi na matokeo ya ziara hizo zote.

### Masharti ya idhini nyingine

Idhini yako haihitajiki kabla ya wilaya ya shule yako haijafanya yafuatayo:

1. inaweza kupitia taarifa iliyopo kama sehemu ya tathmini ya mtoto wako au kufanya upya tathmini; **au**
2. inaweza kumpa mtoto wako mtihani au tathmini nyingine ambayo hutolewa kwa watoto wote isipokuwa kama, kabla ya mtihani au tathmini hiyo, idhini inahitajika kutoka kwa wazazi wote wa watoto wote.

Wilaya ya shule yako haiwezi kutumia kukataa kwako kuidhinisha huduma au shughuli moja kukunyima wewe au mtoto wako huduma, mafao au shughuli nyingine yoyote.

Ikiwa umemwandikisha mtoto wako katika shule binafsi kwa gharama yako mwenyewe au ikiwa unamfundisha mtoto wako nyumbani wewe mwenyewe, na hukutoa idhini yako kwa ajili ya tathmini ya awali ya mtoto wako au kufanyiwa upya tathmini, au unashindwa kujibu ombi la kutoa idhini yako, wilaya ya shule haiwezi kutumia taratibu zake za kubatilisha idhini (yaani, upatanishi, malalamiko yanayostahili, mkutano wa utatuzi, au usikilizwaji wa shauri linalostahili bila upendeleo) na haitakiwi kubaini kama mtoto wako anastahili kupata huduma sawia (huduma zinazotolewa kwa watoto wa shule binafsi wenye ulemavu waliowekwa na wazazi).

**Kuondoa Idhini**

Unaweza kuondoa idhini yako ya utoaji wa elimu maalum na huduma zinazohusiana nayo wakati wowote baada ya utoaji wa awali wa elimu maalum na huduma zinazohusiana nayo kwa mtoto wako. Uondoaji wako wa idhini lazima uwe wa maandishi na huanza kutumika mara baada ya kupokelewa na wilaya ya shule. Mara baada ya kupokelewa uondoaji wako wa idhini wa maandishi, wilaya ya shule:

1. inaweza isiendelee kutoa elimu maalum au huduma zinazohusiana nayo kwa mtoto wako, lakini lazima ikupatie taarifa ya maandishi kabla ya kusitisha utoaji wa elimu na huduma zinazohusiana nayo;
2. haiwezi kutumia upatanishi au taratibu zinazofaa ili kupata makubaliano au uamuzi kwamba elimu maalum na huduma zinazohusiana nayo zitolewe kwa mtoto wako;
3. haitachukuliwa kuwa inakiuka masharti ya kuifanya FAPE ipatikane kwa mtoto wako kwa sababu ya kushindwa kuendelea kumpa mtoto wako elimu maalum na huduma zinazohusiana nayo; **na**
4. haitakiwi kuitisha mkutano wa timu ya IEP au kuiendeleza IEP kwa ajili ya utoaji zaidi wa elimu maalum na huduma zinazohusiana nayo kwa mtoto wako.

## *Wakati gani IEPs lazima Zitumike*

*SBE Rule § 0520-01-09-.13*

IEP ya mtoto wako lazima zitekelezwe haraka iwezekanavyo mara baada ya kukamilishwa. Iwapo makubaliano hayakufikiwa, hakuna mabadiliko katika IEP au hali ya ustahiki ya mtoto wako itakayofanyika kwa siku 14, ili kukupa muda wa kuomba usikilizaji wa shauri linalostahili.

## *Tathmini Huru za Elimu*

*34 C.F.R. § 300.502*

### Jumla

Kama ilivyoelezwa hapa chini, una haki ya kupata Tathmini Huru ya Kielimu (IEE) ya mtoto wako ikiwa hukubaliani na tathmini ya mtoto wako ambayo ilichukuliwa na wilaya ya shule yako.

Ukiomba tathmini huru ya kielimu, wilaya ya shule lazima ikupe taarifa kuhusu mahali unapoweza kupata tathmini huru ya kielimu na kuhusu vigezo vya wilaya ya shule vinavyotumika kwa tathmini huru za kielimu.

### Fasili

*Tathmini ya kujitegemea ya elimu* inamaanisha tathmini inayofanywa na mtahini mwenye sifa ambaye hajaajiriwa na wilaya ya shule inayohusika na elimu ya mtoto wako.

*Gharama ya serikali* inamaanisha kuwa ama wilaya ya shule inalipia gharama yote ya tathmini au inahakikisha kwamba tathmini hiyo inatolewa vinginevyo bila gharama yoyote kutoka kwako, kulingana na masharti ya Sehemu B ya IDEA, ambayo inaruhusu kila jimbo kutumia nyenzo zozote za msaada za jimbo, serikali ya mtaa, serikali kuu na binafsi zinazopatikana katika jimbo ili kukidhi mahitaji ya Sehemu B ya IDEA.

### Haki ya mzazi ya kufanyiwa tathmini kwa gharama ya serikali

Una haki ya tathmini huru ya elimu ya mtoto wako kwa gharama ya serikali ikiwa hukubaliani na tathmini ya mtoto wako iliyofanyika na wilaya ya shule yako, kwa kuzingatia masharti yafuatayo:

1. Ukiomba tathmini huru ya elimu ya mtoto wako kwa gharama ya serikali, wilaya ya shule yako lazima, bila kuchelewa, ama: (a) iwasilishe malalamiko yanayostahili kuomba kusikilizwa ili kuonyesha kwamba tathmini yake kwa mtoto wako inafaa; au (b) kutoa tathmini ya huru ya elimu kwa gharama ya serikali, isipokuwa kama wilaya ya shule itadhihirisha katika kikao cha usikilizaji shauri kuwa tathmini ya mtoto wako uliyopata haikukidhi vigezo vya wilaya ya shule.
2. Ikiwa wilaya ya shule yako itaomba kusikilizwa kwa shauri na uamuzi wa mwisho ni kwamba tathmini ya wilaya ya shule yako kuhusu mtoto wako inafaa, bado una haki ya kufanya tathmini huru ya elimu, lakini sio kwa gharama ya serikali.
3. Ukiomba tathmini huru ya elimu ya mtoto wako, wilaya ya shule inaweza kukuuliza kwa nini unapinga tathmini ya mtoto wako iliyofanywa na wilaya ya shule yako. Hata hivyo, wilaya ya shule yako inaweza isihitaji maelezo na inaweza isichelewe kutoa tathmini huru ya elimu ya mtoto wako kwa gharama ya serikali au kuwasilisha malalamiko yanayostahili ili kuomba usikilizwaji wa shauri ili kutetea tathmini ya wilaya ya shule ya mtoto wako.

Una haki ya kufanya tathmini moja tu huru ya elimu ya mtoto wako kwa gharama ya serikali kila wakati wilaya ya shule yako inapofanya tathmini ya mtoto wako ambayo hukubaliani nayo.

### Tathmini zilizoanzishwa na wazazi

Ukipata tathmini huru ya elimu ya mtoto wako kwa gharama ya serikali au unapoipatia wilaya ya shule tathmini ya mtoto wako ambayo ilifanyika kwa gharama binafsi:

1. wilaya ya shule yako lazima izingatie matokeo ya tathmini ya mtoto wako, ikiwa inakidhi vigezo vya wilaya ya shule vya tathmini huru za elimu, katika uamuzi wowote unaofanywa kuhusiana na utoaji wa Elimu ya Umma Inayofaa Bila Malipo (FAPE) kwa mtoto wako; **na**
2. wewe au wilaya ya shule yako mnaweza kuwasilisha tathmini kama ushahidi katika usikilizaji wa shauri linalostahili kuhusu mtoto wako.

### Maombi ya tathmini yaliyotolewa na mahakimu viongozi

Ikiwa hakimu kiongozi ataomba tathmini huru ya elimu ya mtoto wako kama sehemu ya usikilizaji shauri, gharama ya tathmini hiyo lazima ilipwe na serikali.

**Vigezo vya wilaya ya shule**
Iwapo tathmini ya huru ya elimu inagharamiwa na serikali, vigezo ambavyo tathmini hiyo hupatikana, ni pamoja na eneo la tathmini na sifa za mchunguzi, lazima ziwe sawa na vigezo ambavyo wilaya ya shule hutumia inapoanzisha tathmini (kwa kiwango ambacho vigezo hivyo vinaendana na haki yako ya tathmini huru ya elimu).

Isipokuwa kwa vigezo vilivyoelezwa hapo juu, wilaya ya shule haiwezi kuweka masharti au ratiba zinazohusiana na kupata tathmini huru ya elimu kwa gharama ya serikali.

# Usiri wa Taarifa

## *Fasili*

*34 C.F.R. § 300.611*

Kama ilivyotumika chini ya kichwa cha habari **Usiri wa Taarifa**:

- *Uharibifu* maana yake uharibifu unaoonekana au kuondolewa kwa vitambulisho binafsi kutoka kwenye taarifa ili maelezo yasiwe na utambulisho binafsi tena.
- *Taarifa za elimu* humaanisha aina ya taarifa zinazojumuishwa chini ya fasili ya ''taarifa za elimu'' katika 34 C.F.R. Sehemu ya 99, kanuni zinazotekeleza Sheria ya Haki za Kielimu na Faragha ya Familia ya 1974, 20 U.S.C. 1232g (FERPA).
- *Shirika shiriki* maana yake ni wilaya ya shule, shirika au taasisi yoyote ambayo inakusanya, inahifadhi, au kutumia taarifa zinazomtambulisha mtu, au taarifa ambayo inatolewa, kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA.

## *Taarifa Tambulishi*

*34 C.F.R. § 300.32*

*Taarifa Tambulishi* inamaanisha taarifa ambayo ina:

a) jina la mtoto wako, jina lako kama mzazi, au jina la mwanafamilia mwingine;
b) anwani ya mtoto wako;
c) kitambulisho binafsi, kama vile namba ya hifadhi ya jamii ya mtoto wako au namba ya mwanafunzi; **au**
d) orodha ya sifa bainifu au taarifa nyingine ambayo ingewezesha kumtambua mtoto wako kwa uhakika zaidi.

## *Tangazo kwa Wazazi*

*34 C.F.R. § 300.612*

Wilaya ya shule lazima itoe taarifa ambayo ni toshelevu ili kuwafahamisha wazazi kikamilifu kuhusu usiri wa taarifa tambulishi, ikiwa ni pamoja na:

1. maelezo ya kiwango ambacho taarifa inatolewa katika lugha mama za jamii mbalimbali katika jimbo;
2. maelezo ya watoto ambao taarifa zao tambulishi hutunzwa, aina ya taarifa

zinazotafutwa, njia ambazo serikali inakusudia kutumia katika kukusanya taarifa (pamoja na vyanzo ambako taarifa hizo hukusanywa), na matumizi ya taarifa hizo;
3. muhtasari wa sera na taratibu ambazo mashirika shiriki lazima yafuate kuhusu kuhifadhi, kufichua kwa watu wengine, kuhifadhi na kuharibu taarifa tambulishi; **na**
4. maelezo ya haki zote za wazazi na watoto kuhusu taarifa hii, ikiwa ni pamoja na haki kwa mujibu wa Sheria ya Faragha na Haki za Elimu ya Familia (FERPA) na kanuni zake za utekelezaji katika 34 C.F.R. Sehemu ya 99.

Kabla ya shughuli yoyote kuu ya utambulisho, eneo, au tathmini (pia inajulikana kama "utafutaji wa mtoto"), taarifa lazima ichapishwe au itangazwa katika magazeti au vyombo vingine vya habari, au zote mbili, na mzunguko wa kutosha kuwajulisha wazazi katika hali yote ya shughuli ya kutafuta, kutambua, na kutathmini watoto wanaohitaji elimu maalum na huduma zinazohusiana nayo.

## *Haki ya Kupata Taarifa*

*34 C.F.R. § 300.613*

Shirika shiriki lazima likuruhusu kukagua na kupitia taarifa zozote za elimu zinazohusiana na mtoto wako zinazokusanywa, kutunzwa au kutumiwa na wilaya ya shule yako kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA. Shirika shiriki lazima litii ombi lako la kukagua na kupitia taarifa zozote za elimu za mtoto wako bila kuchelewa na kabla ya mkutano wowote kuhusu Mpango wa Elimu ya Iliobainishwa (IEP), au usikilizaji wowote wa shauri linalostahili usio na upendeleo (pamoja na mkutano wa maazimio au usikilizaji shauri kuhusu nidhamu), na kwa hali yoyote si zaidi ya siku 45 baada ya kuwasilisha ombi.

Haki yako ya kukagua na kupitia taarifa za elimu ini pamoja na:
1. haki yako ya kupata jibu kutoka kwenye shirika shiriki kwa maombi yako yanayofaa kwa ajili ya maelezo na tafsiri za taarifa;
2. haki yako ya kuliomba shirika shiriki kutoa nakala za taarifa ikiwa huwezi kukagua na kupitia ipasavyo taarifa hizo isipokuwa kama umezipokea nakala hizo; **na**
3. haki yako ya kuwa na mwakilishi wako kukagua na kuzipitia taarifa.

Shirika shiriki linaweza kudhania kuwa una mamlaka ya kukagua na kupitia taarifa zinazohusiana na mtoto wako isipokuwa kama imetamkwa kwamba huna mamlaka kwa mujibu wa sheria husika ya jimbo inayosimamia masuala kama vile malezi au kutengana na talaka.

## *Taarifa ya Upatikanaji*

*34 C.F.R. § 300.614*

Kila shirika shiriki lazima liweke kumbukumbu ya wahusika wanaopata ruhusa ya kutumia taarifa za elimu zilizokusanywa, zilizohifadhiwa au zilizotumika kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA (isipokuwa ruhusa ya kutumiwa na wazazi na wafanyikazi walioidhinishwa wa shirika shiriki), ikijumuisha jina la mhusika, tarehe ambayo ruhusa hiyo ilitolewa, na madhumuni ambayo mhusika ameidhinishwa kutumia taarifa hizo.

## *Taarifa Kuhusu Mtoto Zaidi ya Mmoja*

*34 C.F.R. § 300.615*

Iwapo taarifa yoyote ya elimu inajumuisha taarifa kuhusu mtoto zaidi ya mmoja, wazazi wa watoto hao wana haki ya kukagua na kupitia tu taarifa zinazohusiana na mtoto wao au kufahamishwa juu ya taarifa hizo mahususi.

## *Orodha ya Aina na Sehemu za Taarifa*

*34 C.F.R. § 300.616*

Baada ya ombi, kila shirika shiriki lazima likupe orodha ya aina na maeneo zilipo taarifa za elimu zinazokusanywa, kuhifadhiwa au kutumiwa na shirika hilo.

## *Ada*

*34 C.F.R. § 300.617*

Kila shirika shiriki anaweza kutoza ada kwa nakala za taarifa ambazo umetengenezewa kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA, ikiwa ada hiyo haikuzuii kutumia haki yako ya kukagua na kupitia taarifa hizo.

Shirika shiriki haliwezi kutoza ada ya kutafuta au kupata taarifa kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA.

## *Marekebisho ya Taarifa kwa Ombi la Mzazi*

*34 C.F.R. § 300.618 na SBE Rule 0520-01-09-.22*

Iwapo unaamini kwamba taarifa katika kumbukumbu za elimu kuhusu mtoto wako zilizokusanywa, kutunzwa, au kutumika kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA si sahihi, zinapotosha, au zinakiuka faragha au haki nyingine za mtoto wako, unaweza kuliomba shirika shiriki linalotunza taarifa hizo kubadilisha taarifa hizo.

Wilaya ya shule, baada ya kupokea ombi kutoka kwa mzazi kwa mujibu wa 34 C.F.R. § 300.618, itaamua, ndani ya siku kumi 14 za kalenda baada ya kupokea ombi, iwe kurekebisha taarifa kama ilivyoombwa.

Iwapo shirika shiriki litakataa kubadilisha taarifa kulingana na ombi lako, lazima likujulishe kuhusu kukataa na kukushauri kuhusu haki ya kusikilizwa kwa madhumuni haya kama ilivyofafanuliwa chini ya kichwa cha habari ***Fursa ya Kusikilizwa.***

## *Fursa ya Usikilizaji Shauri*

*34 C.F.R. § 300.619*

Shirika shiriki lazima, baada ya kuombwa, likupe fursa ya kusikilizwa ili kupinga taarifa katika kumbukumbu za elimu kuhusu mtoto wako ili kuhakikisha kwamba si sahihi, inapotosha, au vinginevyo inakiuka faragha au haki nyingine za mtoto wako.

## *Taratibu za Usikilizaji Shauri*

*34 C.F.R. § 300.621*

Shauri la kupinga taarifa katika kumbukumbu za elimu lazima liendeshwe kulingana na taratibu za usikilizwaji wa mashauri kama huo kwa mujibu wa Sheria ya Haki za Kielimu na Faragha ya Familia (FERPA).

## *Majibu ya Shauri*

*34 C.F.R. § 300.620*

Iwapo, kutokana na shauri hilo, shirika shiriki litaamua kuwa taarifa hiyo si sahihi, inapotosha au vinginevyo inakiuka faragha au haki nyingine za mtoto, lazima libadilishe ipasavyo taarifa hizo na kukujulisha kwa maandishi.

Iwapo, kutokana na shauri hilo, shirika shiriki litaamua kwamba taarifa hiyo ni sahihi, haipotoshi, au kwa njia nyingine yoyote haikiuki faragha au haki nyingine za mtoto wako, lazima likujulishe kuhusu haki yako ya kuweka kwenye kumbukumbu kwamba inahifadhi kwenye maelezo ya mtoto wako ikielezea kuhusu taarifa hiyo au kutoa sababu zozote ambazo hukubaliani nazo kuhusu uamuzi wa shirika shiriki.

Maelezo kama haya yaliyowekwa kwenye kumbukumbu za mtoto wako lazima:

1. zihifadhiwe na shirika shiriki kama sehemu ya kumbukumbu za mtoto wako ilimradi tu kumbukumbu au sehemu inayogombaniwa inahifadhiwa na shirika shiriki; **na**
2. iwapo shirika shiriki litatoa kumbukumbu za mtoto wako au sehemu inayobishaniwa kwa mhusika mwingine yeyote, maelezo lazima pia yatolewe kwa mhusika huyo.

## *Idhini ya Kutoa Taarifa Zinazoweza Kumtambulisha Mtu*

*34 C.F.R. § 300.622*

Isipokuwa kama taarifa hiyo imo katika kumbukumbu za elimu, na utoaji huo umeidhinishwa bila ridhaa ya mzazi kwa mujibu wa Sheria ya Haki za Kielimu na Faragha ya Familia (FERPA), ni lazima idhini yako ipatikane kabla ya taarifa tambulishi kutolewa kwa wahusika wengine ambao sio maafisa wa mashirika shiriki. Isipokuwa kulingana na hali zilizobainishwa hapa chini, idhini yako haihitajiki kabla ya taarifa ya tambulishi kutolewa kwa maafisa wa mashirika shiriki kwa madhumuni ya kutimiza matakwa ya Sehemu B ya IDEA.

Idhini yako, au idhini ya mtoto anayestahiki ambaye amefikia umri wa miaka inayokubalika kwa mujibu wa sheria ya jimbo, lazima ipatikane kabla ya taarifa tambulishi kutolewa kwa maafisa wa mashirika shiriki yanayotoa au kulipia huduma za mpito.

Ikiwa mtoto wako anasoma, au atasoma, shule binafsi ambayo haiko katika wilaya ya shule unayoishi, ni lazima idhini yako ipatikane kabla ya taarifa zozote tambulishi kuhusu mtoto wako kutolewa kwa maafisa ambao wako katika wilaya ya shule ambako shule binafsi iko na maafisa katika wilaya ya shule unapoishi.

### *Ulinzi*

*34 C.F.R. § 300.623*

Kila shirika shiriki lazima lilinde usiri wa taarifa tambulishi katika hatua za ukusanyaji, uhifadhi, ufichuzi na uharibifu.

Afisa mmoja katika kila shirika shiriki lazima awe na jukumu la kulinda usiri wa taarifa zozote tambulishi.

Watu wote wanaokusanya au kutumia taarifa tambulishi lazima wapate mafunzo au maelekezo kuhusu sera na taratibu za jimbo lako kuhusu usiri kwa mujibu wa Sehemu ya B ya IDEA na Sheria ya Faragha na Haki za Kielimu za Familia (FERPA).

Kila shirika shiriki lazima litunze, kwa ajili ya ukaguzi wa umma, uorodheshaji wa sasa wa majina na nyadhifa za wafanyakazi hao ndani ya shirika ambao wanaweza kuwa na ruhusa ya kupata taarifa tambulishi.

### *Uharibifu wa Taarifa*

*34 C.F.R. § 300.624*

Wilaya ya shule yako lazima ikujulishe pale taarifa tambulishi zinapokuwa zimekusanywa, kuhifadhiwa au kutumiwa kuwa hazihitajiki tena ili kutoa huduma za elimu kwa mtoto wako.

Taarifa lazima iharibiwe baada ya kuomba ifanywe hivyo. Hata hivyo, taarifa ya kudumu ya jina, anwani, na namba ya simu ya mtoto wako, alama zake, kumbukumbu ya mahudhurio, madarasa aliyosoma, darasa alilohitimu, na mwaka aliomaliza unaweza kuhifadhiwa bila kikomo cha muda.

# Taratibu za Malalamiko ya Jimbo na Utatuzi wa Mizozo

### *Tofauti kati ya Taratibu za Malalamiko Yanayostahili Kusikizwa na za Malalamiko ya Kiutawala*

Kanuni za Sehemu B ya IDEA zimeweka utaratibu tofauti wa malalamiko ya kiutawala ya maandishi na kwa ajili ya malalamiko na shauri linalostahili. Kama ilivyoelezwa hapa chini, mtu au shirika lolote linaweza kuwasilisha malalamiko ya kiutawala ya maandishi yanayodai ukiukaji wa masharti yoyote ya Sehemu B yaliyofanywa na wilaya ya shule, Idara ya Elimu ya Tennessee, au shirika lingine lolote la umma. Ni wewe au wilaya ya shule tu mnaoweza kuwasilisha malalamiko yanayostahili kuhusu suala lolote linalohusiana na pendekezo au kukataa kuanzisha au kubadilisha kitambulisho, tathmini au nafasi ya kielimu ya mtoto mwenye ulemavu, au utoaji wa Elimu ya Umma Inayofaa Bila Malipo ( FAPE) kwa mtoto. Ingawa wafanyakazi wa idara kwa ujumla ni lazima watatue malalamiko ya kiutawala kwa maandishi ndani ya kumbukumbu ya matukio ya siku 60, isipokuwa kama muda umeongezwa ipasavyo, hakimu kiongozi lazima asikilize malalamiko yanayostahili (kama hayajatatuliwa kupitia mkutano wa usuluhishi au kupitia upatanishi) na kutoa uamuzi wa

maandishi ndani ya siku 45 baada ya mwisho wa kipindi cha usuluhishi kama ilivyofafanuliwa katika hati hii kwenye kichwa cha habari ***Mchakato wa Usuluhishi***, isipokuwa kama hakimu kiongozi atatoa nyongeza maalum ya ratiba baada ya ombi lako au ombi la wilaya ya shule. Malalamiko ya kiutawala na malalamiko yanayostahili, utatuzi na taratibu za usikilizaji shauri zimefafanuliwa kikamilifu hapa chini.

## *Taratibu za Malalamiko ya Kiutawala*

*34 C.F.R. § 300.151-152 na Mkusanyiko wa Sheria wa Tennessee § 49-10-604*

### Jumla

Idara ya Elimu ya Tennessee, kwa mujibu wa T.C.A. § 49-10-604, itachunguza malalamiko yoyote, ikiwemo malalamiko yaliyowasilishwa na shirika au mtu binafsi. Katika kutatua malalamiko ambayo idara imeona ni kushindwa kutoa huduma zinazofaa, idara itashughulikia:

1. kushindwa kutoa huduma zinazofaa, ikiwa ni pamoja na hatua za marekebisho zinazofaa kushughulikia mahitaji ya mtoto; **na**
2. utoaji wa huduma zinazofaa kwa watoto wote wenye ulemavu.

### Ukomo wa muda; taratibu za chini kabisa

Ndani ya siku 60 baada ya malalamiko kuwasilishwa, idara itafanya yafuatayo:

1. itampa mlalamikaji fursa ya kuwasilisha maelezo ya ziada, ama kwa mdomo au kwa maandishi, kuhusu madai hayo kwenye malalamiko;
2. itaipa wilaya ya shule au shirika lingine la umma fursa ya kujibu malalamiko, ikiwa ni pamoja na, angalau:
   (a) kwa chaguo la shirika, pendekezo la kutatua malalamiko; **na**
   (b) fursa kwa mzazi ambaye amewasilisha malalamiko na shirika ili kukubaliana kwa hiari kushiriki katika upatanishi;
3. kufanya uchunguzi huru kwenye eneo, ikionekana inafaa;
4. kupitia taarifa zote muhimu na kufanya uamuzi huru iwapo wilaya ya shule au shirika lingine la umma linakiuka masharti ya Sehemu B ya IDEA; **na**
5. kutoa uamuzi wa maandishi kwa mlalamikaji ambao unashughulikia kila shitaka katika malalamiko na una:
   (a) uamuzi wa kweli na hitimisho; **na**
   (b) sababu za uamuzi wa mwisho wa idara.

### Kuongeza muda; uamuzi wa mwisho; utekelezaji

Idara itafanya yafuatayo:

1. itaruhusu kuongezwa ukomo wa muda wa siku 60 tu kama:
   a. hali za kipekee zipo pamoja na malalamiko mahususi; **au**
   b. mzazi na wilaya ya shule au shirika lingine la umma linalohusika linakubali kwa hiari kuongeza muda wa kutatua suala hilo kupitia upatanishi au njia mbadala za utatuzi wa migogoro.
2. kutoa, ikihitajika: (a) shughuli za msaada wa kiufundi; (b) mazungumzo; **na** (c) hatua za masahihisho ili kufikia maridhiano.

**Malalamiko ya jimbo na usikilizaji wa shauri linalostahili**
Ikiwa malalamiko ya kiutawala yatapokelewa ambayo pia yanahusu shauri linalostahili kama ilivyofafanuliwa hapa chini kwa kichwa cha habari ***Kuwasilisha Malalamiko Yanayostahili***, au malalamiko yana masuala mengi ambayo moja au zaidi ni sehemu ya shauri hili, idara itapanga malalamiko ya kiutawala au sehemu yoyote ya malalamiko ambayo yanashughulikiwa katika shauri linalistahili hadi usikilizaji wa shauri unapokamilika. Suala lolote lililo katika malalamiko ya utawala ambalo si sehemu ya shauri linalostahili litatuliwe kwa kutumia ukomo wa muda na taratibu zilizoelezwa hapo juu.

Iwapo suala lililoibuliwa katika malalamiko ya kiutawala limeamuliwa hapo awali katika shauli linalostahili linalohusisha wahusika walewale (wewe na wilaya ya shule), basi uamuzi wa shauri hilo unahusisha suala hilo.

Malalamiko ya kiutawala yanayodai kushindwa kwa wilaya ya shule au shirika lingine la umma kutekeleza uamuzi wa shauri linalostahili lazima yatatuliwe na idara.

## *Muwasilisha Malalamiko*

*34 C.F.R. § 300.153 na Mkusanyiko wa Sheria za Tennessee § 49-10-604*

Shirika au mtu binafsi anaweza kuwasilisha malalamiko ya kiutawala yaliyotiwa saini kwa mujibu wa taratibu zilizoelezwa hapo juu.

Malalamiko ya maandishi lazima yajumuishe:

1. taarifa kwamba wilaya ya shule au shirika lingine la umma limekiuka masharti ya Sehemu B ya IDEA au kanuni zake;
2. ukweli ambao maelezo hayo umejikita kwayo;
3. sahihi na taariza za mawasiliano ya mlalamikaji; na
4. ikiwa ukiukaji unaoshukiwa unamhusu mtoto maalum:
    a. jina la mtoto na anwani ya makazi ya mtoto;
    b. jina la shule ambayo mtoto anasoma;
    c. iwapo ni mtoto au kijana asiye na makazi, taarifa zilizopo za mawasiliano kwa mtoto, na jina la shule ambayo mtoto anasoma;
    d. maelezo ya asili ya tatizo la mtoto, pamoja na ukweli unaohusiana na tatizo hilo; **na**
    e. suluhu iliyopendekezwa kuhusu tatizo kwa kiwango kinachojulikana na kinachopatikana kwa upande unaowasilisha malalamiko wakati malalamiko hayo yanawasilishwa.

Malalamiko lazima yadai ukiukaji uliotokea si zaidi ya mwaka mmoja kupita kabla ya tarehe ambayo malalamiko yamepokelewa.

Upande unaowasilisha malalamiko ya kiutawala ya maandishi lazima upeleke nakala ya malalamiko kwenye wilaya ya shule au shirika lingine la umma linalomhudumia mtoto wakati huohuo upande huo uwasilishe malalamiko hayo kwenye Idara ya Elimu ya Tennessee.

## *Fomu za Mfano*

*34 C.F.R. § 300.509*

Idara ya Elimu ya Tennessee imeunda fomu ya itakayokusaidia kuwasilisha malalamiko ya kiutawala ya maandishi. Fomu hii imejumuishwa nyuma ya kijitabu hiki.

## *Upatanishi*

*34 C.F.R. § 300.506 na Mkusanyiko wa Sheria za Tennessee § 49-10-605*

### Jumla

Wilaya ya shule lazima ihakikishe upatanishi unapatikana ili kukuwezesha wewe na wilaya ya shule kutatua mgogoro wa jambo lolote kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA, ikiwemo masuala yanayotokea kabla ya kuwasilisha malalamiko yanayostahili. Hivyo, upatanishi unapatikana ili kutatua mizozo kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA, iwe umewasilisha malalamiko yanayostahili au la ili kuomba kusikilizwa kwa shauri hilo kama ilivyofafanuliwa kwenye kichwa cha habari ***Kuwasilisha Malalamiko Yanayostahili***.

### Masharti

Taratibu lazima zihakikishe kwamba mchakato wa upatanishi:

1. ni wa hiari kwa upande wako na kwa upande wa wilaya ya shule;
2. hazitumiki kunyima au kuchelewesha haki yako ya kusikiliza shauri linalostahili, au kukunyima haki nyingine yoyote uliyo nayo kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA; **na**
3. unaendeshwa na mpatanishi mwenye sifa na asiye na upendeleo ambaye amepokea mafunzo ya mbinu bora za upatanishi.

Wilaya ya shule inaweza kuunda taratibu zinazowapa wazazi na shule ambazo zimeamua kutotumia mchakato wa upatanishi, fursa ya kukutana, kwa wakati na eneo linalokufaa, na mtu asiyenufaika na shauri hilo:

1. ambaye yuko chini ya mkataba na taasisi inayofaa ya usuluhishi wa mizozo, kituo cha mafunzo na taarifa kwa wazazi, au kituo cha taarifa kwa wazazi katika jimbo; **na**
2. ambaye ataeleza faida na kuhimiza matumizi ya mchakato wa upatanishi kwako.

Idara ya Elimu ya Tennessee inawajibika kwa gharama ya mchakato wa upatanishi, ikiwa ni pamoja na gharama za mikutano.

Kila mkutano katika mchakato wa upatanishi lazima uratibiwe kwa wakati unaofaa na ufanyike mahali panapokufaa wewe na wilaya ya shule.

Ikiwa wewe na wilaya ya shule mtasuluhisha mzozo kupitia mchakato wa upatanishi, pande zote mbili lazima ziingie katika makubaliano ya kisheria ambayo yataweka azimio hilo na ambayo:

1. yaseme kwamba majadiliano yote yaliyofanyika wakati wa mchakato wa upatanishi yatabaki kuwa siri na hayawezi kutumika kama ushahidi katika kusikilizwa kwa mchakato wowote unaofuata au shauri la madai; **na**
2. yamesainiwa na na pande zote mbili wewe na mwakilishi wa wilaya ya shule ambaye ana mamlaka ya kufuatwa na wilaya ya shule.

Majadiliano yaliyotokea wakati wa mchakato wa upatanishi lazima yawe ya siri. Hayawezi kutumika kama ushahidi katika usikilizwaji wa shauri linalostahili wa siku zijazo au kesi ya madai ya mahakama yoyote ya serikali kuu au mahakama ya jimbo inayopokea msaada kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA.

#### Mpatanishi kutokuwa na upendeleo

Mpatanishi:

1. anaweza asiwe mwajiriwa wa Idara ya Elimu ya Tennessee au wilaya ya shule inayohusika na elimu au malezi ya mtoto wako; **na**
2. lazima asiwe na maslahi binafsi au ya kitaaluma ambayo yanapingana na lengo la mpatanishi.

Mtu ambaye anastahiki vinginevyo kuwa mpatanishi si mwajiriwa wa wilaya ya shule au shirika la jimbo kwa sababu tu analipwa na shirika au wilaya ya shule kuhudumu kama mpatanishi.

## *Fomu za Mfano*

*34 C.F.R. § 300.509*

Idara ya Elimu ya Tennessee imeunda fomu ya kukusaidia kuomba upatanishi. Fomu hii imejumuishwa nyuma ya kijitabu hiki.

## *Taratibu za Malalamiko Yanayostahili*

## *Kuwasilisha Malalamiko Yanayostahili*

*34 C.F.R. § 300.507 na Mkusanyiko wa Sheria za Tennessee § 49-10-606*

#### Jumla

Wewe au wilaya ya shule mnaweza kuwasilisha malalamiko ya yanaostahili kuhusu suala lolote linalohusiana na pendekezo au kukataa kuanzisha au kubadilisha kitambulisho, tathmini, au nafasi ya kielimu ya mtoto wako au utoaji wa Elimu ya Umma Inayofaa Bila Malipo (FAPE) kwa mtoto wako.

Malalamiko yanayostahili lazima yadai ukiukaji uliotokea si zaidi ya miaka miwili kabla wewe au wilaya ya shule kujua au kujulikana kwa hatua inayodaiwa ambayo ni msingi wa malalamiko yanayostahili.

Ratiba ya hapo juu haikuhusu iwapo hukuweza kuwasilisha malalamiko yanayostahili ndani ya muda uliopangwa kwa sababu:

1. wilaya ya shule iliwakilisha vibaya kwamba ilikuwa imesuluhisha maswala yaliyoainishwa kwenye malalamiko; **au**
2. wilaya ya shule ilizuia taarifa kutoka kwako ambayo ilipaswa ikupe kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA.

#### Taarifa kwa wazazi

Wilaya ya shule lazima ikujulishe kuhusu huduma zozote za kisheria za bure au za gharama nafuu na nyinginezo zinazofaa zinazopatikana katika eneo hilo ikiwa unaomba taarifa hiyo **au** ikiwa wewe au wilaya ya shule itawasilisha malalamiko yanayostaili.

## *Malalamiko Yanayostahili*

*34 C.F.R. §§ 300.507-508*

### Jumla

Ili kuomba kusikilizwa kwa shauri, wewe au wilaya ya shule (au wakili wako au wakili wa wilaya ya shule) lazima iwasilishe malalamiko yanayostahili kwa upande mwingine. Malalamiko hayo lazima yawe na maudhui yote yaliyoorodheshwa hapa chini na lazima yawe siri.

Wewe au wilaya ya shule, yeyote aliyewasilisha malalamiko, lazima pia aipe Idara ya Elimu ya Tennessee nakala ya malalamiko.

### Maudhui ya malalamiko

Malalamiko yanayostahili lazima yajumuishe:

1. jina la mtoto;
2. anwani ya makazi ya mtoto;
3. jina la shule ya mtoto;
4. ikiwa mtoto ni mtoto au kijana asiye na makazi, taarifa ya mawasiliano ya mtoto na jina la shule ya mtoto;
5. maelezo ya asili ya tatizo la mtoto linayohusiana na hatua iliyopendekezwa au iliyokataliwa, pamoja na ukweli unaohusiana na tatizo hilo; **na**
6. utatuzi uliopendekezwa wa tatizo kwa kiwango kinachojulikana na kupatikana kwako au wilaya ya shule wakati huo.

### Taarifa inahitajika kabla ya usikilizaji wa shauri kwenye malalamiko yanayostahili

Wewe au wilaya ya shule huenda msiwe na shauri la kusikilizwa hadi wewe au wilaya ya shule (au wakili wako au wakili wa wilaya ya shule) iwasilishe malalamiko yanayostahili ambayo yanajumuisha maelezo yaliyoorodheshwa hapo juu.

### Utoshelevu wa malalamiko

Ili malalamiko yanayostahili kuendelea, ni lazima yachukuliwe kuwa yanatosha. Malalamiko yanayostahili yatachukuliwa kuwa yanatosha (ikiwa yamekidhi mahitaji ya maudhui yaliyo hapo juu) isipokuwa kama mhusika anayepokea malalamiko yanayostahili (wewe au wilaya ya shule) atamjulisha hakimu kiongozi na mhusika mwingine—kwa maandishi na ndani ya siku 15 baada ya kupokea malalamiko—kwamba mhusika anayepokea anaamini kwamba malalamiko yanayostahili hayakidhi mahitaji yaliyoorodheshwa hapo juu.

Ndani ya siku tano baada ya kupokea taarifa, mhusika anayepokea (wewe au wilaya ya shule) atachukulia kuwa malalamiko yanayostahili kuwa hayana msingi, hakimu kiongozi lazima aamue kama malalamiko hayo yanakidhi masharti yaliyoorodheshwa hapo juu na akujulishe wewe na wilaya ya shule kwa maandishi haraka.

### Marekebisho ya malalamiko

Wewe au wilaya ya shule mnaweza kufanya mabadiliko kwenye malalamiko iwapo tu:

1. upande mwingine unaidhinisha mabadiliko hayo kwa maandishi na kupewa nafasi ya kutatua malalamiko hayo kupitia mkutano wa maazimio; **au**

2. kabla ya siku tano kupita kabla ya kuanza kusikilizwa kwa shauri hilo, hakimu kiongozi hutoa ruhusa kwa ajili ya mabadiliko hayo.

Iwapo mlalamikaji (wewe au wilaya ya shule) atafanya mabadiliko kwenye malalamiko, ratiba za mkutano wa utatuzi (ndani ya siku 15 baada ya kupokea malalamiko) na muda wa utatuzi (ndani ya siku 30 baada ya kupokea malalamiko hayo) huanza tena tarehe ambayo malalamiko yaliyorekebishwa yanawasilishwa.

**Jibu la Shirika la Elimu la Serikali ya Mitaa (LEA) au la wilaya ya shule kwa malalamiko hayo**

Iwapo wilaya ya shule haijatuma taarifa ya awali kwako, kama ilivyobainishwa katika kichwa cha habari ***Taarifa ya Awali ya Maandishi***, kuhusu lililo katika malalamiko yako, wilaya ya shule lazima, ndani ya siku 10 baada ya kupokea malalamiko hayo, ikutumie jibu linalojumuisha:

1. maelezo ya kwa nini wilaya ya shule ilipendekeza au ilikataa kuchukua hatua iliyowasilishwa katika malalamiko hayo;
2. maelezo ya machaguo mengine ambayo timu ya Mpango wa Elimu Iliyopambanuliwa (IEP) ya mtoto wako ilizingatia na sababu zilizofanya machaguo hayo kukataliwa;
3. maelezo ya kila utaratibu wa tathmini, tathmini, rekodi, au ripoti ya wilaya ya shule iliyotumiwa kama msingi wa hatua iliyopendekezwa au kukataliwa; **na**
4. maelezo ya vipengele vingine vinavyohusiana na hatua iliyopendekezwa au iliyokataliwa na wilaya ya shule.

Kutoa taarifa katika vipengele 1–4 hapo juu hakuizuii wilaya ya shule kudai kwamba malalamiko yako hayana msingi.

**Majibu ya upande mwingine kwa malalamiko hayo**

Isipokuwa kama ilivyoelezwa katika kichwa cha habari kidogo hapo juu, ***Shirika la Elimu la Serikali ya Mitaa* (*LEA) au jibu la wilaya ya shule kwa malalamiko hayo***, mhusika anayepokea malalamiko hayo lazima, atume majibu ambayo yanashughulikia maswala maalum katika malalamiko kwa mhusika ndani ya siku 10 baada ya kupokea malalamiko hayo.

## *Fomu za Mfano*

*34 C.F.R. § 300.509*

Idara ya Elimu ya Tennessee imeunda fomu itakayokusaidia kuomba kusikilizwa shauri. Fomu hii imejumuishwa nyuma ya kijitabu hiki.

## *Mchakato wa Kumpanga Darasa Mtoto Unasubiri Shauri Kusikilizwa*

*34 C.F.R. § 300.518*

Isipokuwa kama ilivyoainishwa katika kichwa cha habari ***Taratibu za Kuwaadhibu Watoto Wenye Ulemavu,*** mara baada ya malalamiko kutumwa kwenda mhusika mwingine, katika kipindi cha mchakato wa utatuzi, na wakati wa kusubiri uamuzi wa shauri hilo au taratibu za kimahakama, isipokuwa kama wewe na wilaya ya shule inakubali vinginevyo, mtoto wako lazima abaki katika nafasi yake ya sasa ya elimu.

Iwapo malalamiko hayo yanahusisha maombi ya uandikishwaji wa awali kwenye shule ya umma, mtoto wako, kwa idhini yako, lazima awekwe katika mpango wa kawaida wa shule ya umma hadi pale shauri hilo litakapokamilika.

Iwapo malalamiko hayo yanahusisha maombi ya huduma za awali kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA kwa mtoto anayehama kutoka kuhudumiwa kwa mujibu wa Sehemu C ya IDEA kwenda Sehemu B ya IDEA na ambaye hastahiki tena huduma za Sehemu C kwa sababu mtoto ametimiza miaka mitatu, wilaya ya shule haipaswi kutoa huduma za Sehemu C ambazo mtoto amekuwa akipokea. Iwapo mtoto ameonekana kuwa anastahili kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA na unakubali mtoto kupokea elimu maalum na huduma zinazohusiana nayo kwa mara ya kwanza, basi, wakati unasubiri matokeo ya kesi, wilaya ya shule lazima itoe elimu hiyo maalum na huduma zinazohusiana nayo ambayo haimo kwenye mgogoro (yale ambayo wewe na wilaya ya shule mnakubaliana).

## *Mchakato wa Upatanisho*

*34 C.F.R. § 300.510*

**Mkutano wa usuluhishi**

Ndani ya siku 15 baada ya kupokea taarifa ya malalamiko yako na kabla ya kusikilizwa kwa shauri hilo, wilaya ya shule lazima iitishe mkutano utakaokushirikisha wewe na na mjumbe husika au wanatimu wa Mpango wa Elimu Iliyopambanuliwa (IEP) ambao wana ujuzi maalum wa ukweli uliobainishwa kwenye malalamiko yako. Mkutano:

1. lazima ijumuishe mwakilishi wa wilaya ya shule ambaye ana mamlaka ya kufanya maamuzi kwa niaba ya wilaya ya shule; **na**
2. haiwezi kujumuisha wakili wa wilaya ya shule isipokuwa kama umeandamana na wakili.

Wewe na wilaya ya shule mtaamua washiriki husika wa timu ya IEP watakaohudhuria mkutano huo.

Madhumuni ya mkutano huo ni kwa ajili ya kujadili malalamiko yako na ukweli unaounda msingi wa malalamiko ili wilaya ya shule ipate fursa ya kutatua mgogoro huo.

Mkutano wa utatuzi sio lazima ikiwa:

1. wewe na wilaya ya shule mnakubali kwa maandishi kuahirisha mkutano huo; **au**
2. wewe na wilaya ya shule mnakubali kutumia mchakato wa upatanishi, kama ilivyofafanuliwa katika kichwa cha habari ***Upatanishi***.

**Kipindi cha utatuzi**

Ikiwa wilaya ya shule haijasuluhisha malalamiko hayo kwa kiwango cha kukuridhisha ndani ya siku 30 baada ya kupokea malalamiko hayo (wakati wa muda wa mchakato wa utatuzi), usikilizwaji wa shauri unaweza kutokea.

Ratiba ya siku 45 ya kutoa uamuzi wa mwisho huanza baada ya kumalizika kwa muda wa usuluhishi wa siku 30, isipokuwa katika hali fulani za marekebisho yaliyofanywa kwa kipindi cha siku 30, kama ilivyoelezwa hapa chini.

Isipokuwa pale ambapo wewe na wilaya ya shule mmekubali kuahirisha mchakato wa usuluhishi au kutumia upatanishi, kushindwa kwako kushiriki katika mkutano wa usuluhishi kutacheleweesha muda wa mchakato wa usuluhishi na usikilizwaji wa shauri hadi pale utakapokubali kushiriki katika mkutano.

Baada ya kufanya juhudi zinazofaa na kuweka kumbukumbu za juhudi hizo, wilaya ya shule haiwezi kupata ushiriki wako katika mkutano wa usuluhishi, wilaya ya shule inaweza, mwishoni mwa kipindi cha usuluhishi cha siku 30, kuomba kwamba hakimu kiongozi atupilie mbali malalamiko yako. Nyaraka za juhudi hizo lazima zijumuishe taarifa ya majaribio ya wilaya ya shule kupanga muda na mahali palipokubaliwa na pande zote mbili, kama vile:

1. taarifa ya kina ya miito ya simu iliyofanyika au iliyojaribiwa na majibu ya kupiga huko simu
2. Nakala za barua zilizotumwa kwako na majibu yoyote yaliyopokelewa
3. Taarifa za kina za ziara zilizofanyika kuja nyumbani kwako au mahali pa kazi na matokeo ya ziara hizo

Iwapo wilaya ya shule itashindwa kuitisha mkutano wa usuluhishi ndani ya siku 15 baada ya kupokea taarifa ya malalamiko yako **au** inashindwa kushiriki katika mkutano wa usuluhishi, unaweza kumwomba hakimu kiongozi kuamuru kwamba usikilizaji wa shauri la siku 45 uanze.

### Marekebisho ya kipindi cha usuluhishi kuwa siku 30

Iwapo wewe na wilaya ya shule mnakubali kwa maandishi kuacha mkutano wa usuluhishi, basi ratiba ya siku 45 ya usikilizaji wa shauri hilo uanze siku inayofuata.

Baada ya kuanza kwa mkutano wa upatanishi au usuluhishi na kabla ya mwisho wa kipindi cha usuluhishi cha siku 30, ikiwa wewe na wilaya ya shule mnakubaliana kwa maandishi kwamba hakuna makubaliano yanayowezekana, basi ratiba ya siku 45 usikilizaji wa shauri huanza siku inayofuata.

Ikiwa wewe na wilaya ya shule mnakubali kutumia mchakato wa upatanishi, mwishoni mwa kipindi cha usuluhishi cha siku 30, pande zote mbili zinaweza kukubaliana kwa maandishi kuendelea na upatanishi hadi makubaliano yafikiwe. Hata hivyo, iwapo wewe au wilaya ya shule mtajiondoa kwenye mchakato wa upatanishi, basi ratiba ya siku 45 ya usikilizaji wa shauri hilo itaanza siku inayofuata.

### Makubaliano ya usuluhishi wa maandishi

Ikiwa suluhu ya mzozo itafikiwa katika mkutano wa usuluhishi, wewe na wilaya ya shule lazima muingie katika makubaliano ya kisheria ambayo:

1. yamesainiwa na wewe na mwakilishi wa wilaya ya shule ambaye ana mamlaka ya kufuatwa na wilaya ya shule; **na**
2. yanatekelezeka katika mahakama yoyote ya jimbo yenye mamlaka husika (mahakama ya jimbo ambayo ina mamlaka ya kusikiliza kesi ya aina hii) **au** katika mahakama ya wilaya ya Marekani **au** na shirika la elimu la jimbo (ikiwa jimbo lako lina utaratibu au taratibu nyingine zinazoruhusu wahusika kutafuta utekelezaji wa makubaliano ya usuluhishi).

#### Kipindi cha mapitio ya makubaliano

Iwapo wewe na wilaya ya shule mnaingia katika makubaliano kutokana na mkutano wa usuluhishi, upande wowote (wewe au wilaya ya shule) unaweza kubatilisha makubaliano hayo ndani ya siku tatu (3) za kazi baada ya wewe na wilaya ya shule kutia sahihi makubaliano huo.

## *Usikilizaji wa Shauri Unaostahili*

*34 C.F.R. § 300.511 na Mkusanyiko wa Sheria za Tennessee § 49-10-606*

### Jumla

Wakati wowote malalamiko yanapowasilishwa, wewe au wilaya ya shule inayohusika katika mgogoro lazima iwe na fursa ya kusikilizwa katika shauri bila upendeleo, kama ilivyoelezwa katika sehemu za ***Malalamiko Yanayostahili*** na ***Mchakato wa Usuluhishi***.

#### Hakimu kiongozi

Kwa uchache, hakimu kiongozi:

1. hapaswi kuwa mwajiriwa wa Idara ya Elimu ya Tennessee au wilaya ya shule inayohusika na elimu au malezi ya mtoto (Hata hivyo, mtu hawi mwajiriwa wa shirika kwa sababu tu analipwa na shirika kuhudumu kama hakimu kiongozi);
2. lazima asiwe na maslahi binafsi au ya kitaaluma ambayo yanakinzana na usawa wa hakimu kiongozi katika usikilizaji wa shauri hilo;
3. lazima awe na ujuzi na aelewe masharti ya IDEA, na kanuni za serikali kuu na jimbo zinazohusiana na IDEA, na tafsiri za kisheria za IDEA na mahakama za serikali kuu na za jimbo; **na**
4. lazima awe na ujuzi na uwezo wa kuendesha kesi, na kufanya na kuandika uamuzi, kulingana na kanuni zinazofaa za kisheria.

#### Mada ya Shauri Linalohusika

Mhusika (wewe au wilaya ya shule) anayeomba shauri lisikilizwe hawezi kuibua matatizo wakati wa usikilizaji wa shauri ambayo hayakushughulikiwa wakati wa ushughulikiaji wa malalamiko, isipokuwa kama mhusika mwingine atakubali.

#### Muda wa kuomba usikilizaji wa shauri

Wewe au wilaya ya shule lazima iombe usikilizaji usio na upendeleo wakati wa usikilizaji wa malalamiko yanayostahili ndani ya miaka miwili tokea tarehe ambayo wewe au wilaya ya shule mlijua au mngejua kuhusu suala lililoshughulikiwa katika malalamiko.

#### Vitu vinavyosamehewa katika ratiba

Ratiba ya hapo juu haikuhusu ikiwa hukuweza kuwasilisha malalamiko yanayostahili kwa sababu ya yafuatayo:

1. Wilaya ya shule iliwakilisha vibaya kwamba ilikuwa imesuluhisha tatizo au suala ambalo unalileta katika malalamiko yako.
2. Wilaya ya shule ilizuia taarifa ambazo ulipaswa kupewa kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA.

## *Haki za Usikilizaji wa Shauri*

*34 C.F.R. § 300.512*

### Jumla

Mhusika yeyote katika usikilizaji wa shauri (ikiwemo shauri linaohusiana na taratibu za kinidhamu) ana haki ya:

1. kusindikizwa na kushauriwa na mwanasheria na/au watu wenye ujuzi au mafunzo maalum kuhusu matatizo ya watoto wenye ulemavu;
2. kuwasilisha ushahidi na kukabiliana, kuhoji, na kuhitaji mahudhurio ya mashahidi;
3. kukataza kutolewa kwa ushahidi wowote katika kesi ambao haujatolewa kwa upande huo angalau siku tano za kazi kabla ya kusikilizwa;
4. kupata nakala ya maandishi, au, ya chaguo lako, kielekroniki, rekodi ya neno kwa neno shauri hilo; **na**
5. kupata nakala ya maandishi, au, ya muundo uupendao, ya kielektroniki ya majibu ya ukweli na uamuzi.

### Utoaji wa ziada wa taarifa

Angalau siku tano za kazi kabla ya usikilizaji wa shauri hilo, wewe na wilaya ya shule lazima mpeane tathmini zote zilizokamilika kabla ya tarehe hiyo na mapendekezo kulingana na tathmini hizo ambazo wewe au wilaya ya shule mnakusudia kuzitumia kwenye shauri.

Hakimu kiongozi anaweza kuuzuia upande wowote ambao hautatii masharti haya ya kuwasilisha tathmini au pendekezo husika kwenye kikao bila idhini ya upande mwingine.

### Haki za mzazi wakati wa kusikiliza shauri

Lazima upewe haki ya:

1. kuhakikisha mtoto anakuwepo;
2. kufungua shauri kwa umma; **na**
3. kuwa na kumbukumbu za shauri, matokeo ya kesi, na upatiwe uamuzi wa shauri bila gharama yoyote.

## *Maamuzi ya Shauri*

*34 C.F.R. § 300.513*

### Uamuzi wa hakimu kiongozi

Uamuzi wa hakimu kiongozi kuhusu iwapo mtoto wako alipata Elimu ya Umma Inayofaa Bila Malipo (FAPE) lazima itajikita kwenye sababu ya msingi.

Iwapo madai yanahusu ukiukaji wa utaratibu, hakimu kiongozi anaweza kubaini kwamba mtoto wako hajapata FAPE ikiwa tu mapungufu ya utaratibu:

1. uliingilia haki ya mtoto wako ya Elimu Umma Inayofaa Bila Malipo (FAPE);
2. iliingilia kwa kiasi kikubwa fursa yako ya kushiriki katika mchakato wa kufanya maamuzi kuhusu utoaji wa Elimu ya Umma Inayofaa Bila Malipo (FAPE) kwa mtoto wako; **au**
3. kusababisha kunyimwa faida ya kielimu.

**Ibara ya ujenzi**
Hakuna masharti kati ya yaliyoelezwa hapo juu yanayoweza kufasiriwa ili kumzuia hakimu kiongozi kuiamuru wilaya ya shule kutii masharti yaliyo katika ibara ya ulinzi wa haki za mtoto mwenye ulemavu na wazazi wake ya kanuni za serikali kuu kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA (34 C.F.R. §§ 300.500 hadi 300.536).

**Ombi tofauti la shauri linalostahili**
Hakuna kitu chochote ibara ya ulinzi wa wa haki za watoto wenye ulemavu na wazazi wao ya
kanuni za serikali kuu kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA (34 C.F.R. §§ 300.500 hadi 300.536) inaweza kufasiriwa ili kukuzuia kuwasilisha malalamiko tofauti kuhusu masuala tofauti na malalamiko ambao tayari yamewasilishwa.

**Matokeo na uamuzi kwa jopo la ushauri na umma kwa ujumla**
Idara, baada ya kufuta taarifa zozote tambulishi, lazima:

1. itoe matokeo na maamuzi katika usikilizaji wa kesi au ikate rufaa kwenye jopo maalum la ushauri wa kielimu la jimbo; **na**
2. ihakikishe matokeo na maamuzi hayo yanapatikana kwa umma.

## *Rufaa*

*34 C.F.R. § 300.514*

**Mwisho wa uamuzi wa shauri**
Uamuzi unaotolewa wakati wa usikilizaji wa shauri (ikiwemo shauri linalohusiana na taratibu za kinidhamu) ni wa mwisho, isipokuwa kwamba upande wowote unaohusika katika shauri hilo (wewe au wilaya ya shule) unaweza kukata rufaa dhidi ya uamuzi huo kwa kuleta kesi ya madai.

## *Ratiba ya matukio*

*34 C.F.R. § 300.515*

Isiwe zaidi ya siku 45 baada ya kumalizika kwa muda wa siku 30 wa mikutano ya usuluhishi, **au** kama ilivyofafanuliwa katika kichwa kidogo cha habari ***Marekebisho ya kipindi cha usuluhishi hadi siku 30***, zisizidi siku 45 baada ya kumalizika kwa muda wa siku 30 za muda uliorekebishwa:

1. Uamuzi wa mwisho umefikiwa katika kesi
2. Nakala ya uamuzi huo inatumwa kwa kila mhusika

Hakimu kiongozi anaweza kutoa nyongeza maalum ya muda zaidi ya muda wa siku 45 iliyobainishwa hapo juu mara baada ya kuombwa na upande wowote.

Kila shauri lazima liendeshwe kwa wakati na mahali panapokufaa wewe na mtoto wako.

## *Hatua za Kiraia*

*34 C.F.R. § 300.516*

### Jumla

Upande wowote (wewe au wilaya ya shule) ambao haukubaliani na matokeo na uamuzi wa shauri hilo (ikiwemo shauri linalohusiana na taratibu za kinidhamu) una haki ya kufungua kesi ya madai kuhusiana na suala ambalo lilikuwa linahusiana na shuari hilo. Hatua hiyo inaweza kuletwa katika baraza la mahakama kuu ya jimbo au mahakama ya mzunguko au katika mahakama ya wilaya ya Marekani bila kujali kiasi cha mzozo.

#### Ukomo wa muda

Mhusika (wewe au wilaya ya shule) anayefungua kesi atakuwa na siku 60 kuanzia tarehe ya uamuzi wa hakimu kiongozi kuwasilisha kesi yake ya madai.

#### Taratibu za ziada

Katika kila kesi ya madai, mahakama:

1. hupokea kumbukumbu za mashauri ya utawala;
2. husikiliza ushahidi wa ziada unapoomba au wilaya ya shule inapoomba; **na**
3. hutoa uamuzi wake kwa kuzingatia wingi wa ushahidi na hutoa misaada ambayo mahakama huoana kuwa inafaa.

#### Mamlaka ya mahakama za wilaya

Mahakama za wilaya za Marekani zina mamlaka ya kutoa uamuzi kuhusu hatua zinazoletwa kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA bila kujali kiasi kinachobishaniwa.

#### Kanuni ya ujenzi

Hakuna kitu chochote katika Sehemu B ya IDEA inayozuia au kuweka kikomo cha haki, taratibu, na suluhu zinazopatikana kwa mujibu wa Katiba ya Marekani, Sheria ya Wamarekani Wenye Ulemavu ya 1990, Sura ya V ya Sheria ya Ukarabati ya 1973 (Sehemu ya 504), au sheria zingine za serikali kuu zinazolinda haki za watoto wenye ulemavu, isipokuwa kwamba kabla ya kuwasilishwa kwa kesi ya madai kwa mujibu wa sheria hizi kutafuta afueni ambayo inapatikana pia kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA, taratibu shauri linalostahili zilizoelezwa hapo juu lazima zitumike kwa kiwango sawa na ambacho kingehitajika kama upande uliowasilisha kesi kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA. Hii ina maana kwamba unaweza kupata suluhu katika sheria zingine zinazoingiliana na zile zinazopatikana kwa mujibu wa IDEA, lakini kwa ujumla, ili kupata unafuu kwa mujibu wa sheria hizo nyingine, lazima kwanza utumie suluhu ya kiutawala inayopatikana kwa mujibu wa IDEA (yaani, malalamiko yanayostahili, mkutano wa usuluhishi, na taratibu za kusikiliza mashauri bila upendeleo) kabla ya kwenda moja kwa moja mahakamani.

## *Ada ya Mwanasheria*

*34 C.F.R. § 300.517*

### Jumla

Katika hatua yoyote au shauri lililoletwa kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA, ikiwa utashinda, mahakama, kwa uamuzi wake, inaweza kukupa kiasi fulani kwa ajili ya ada za mawakili kama sehemu ya gharama zako.

Katika hatua au shauri lolote lililoletwa kwa mujibu Sehemu B ya IDEA, mahakama, kwa uamuzi wake, inaweza kutoa kiasi fulani cha fedha kama ada za mawakili kama sehemu ya gharama za wilaya ya shule ambacho kitalipwa na wakili wako ikiwa wakili: (a) aliwasilisha malalamiko au kesi mahakamani ambayo mahakama inaona haina mashiko, haina maana, au haina msingi; **au** (b) aliendelea kushtaki baada ya shauri hilo kuonekana halina mashiko, halina maana, au halina msingi.

Katika hatua au shauri lolote lililoletwa kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA, mahakama, kwa uamuzi wake, inaweza kuamuru kiasi fulani cha fedha kilipwe kama ada za mawakili kama sehemu ya gharama ambazo wilaya ya shule ilitumia ambacho utapaswa kulipa wewe au wakili wako iwapo uliomba usikilizaji wa shauri au kesi mahakamani hapo baadaye iliwasilishwa kwa madhumuni yoyote yasiyofaa, kama vile kufanya vurumai, kusababisha ucheleweshaji usio wa lazima, au kuongeza gharama ya shauri au kesi.

**Utoaji wa ada**

Mahakama hutoza ada zinazofaa za mawakili kama ifuatavyo:

1. Ada lazima zitozwe kulingana na viwango vilivyopo katika jamii ambayo shauri au kesi hiyo imefanyika kulingana na aina na ubora wa huduma zinazotolewa. Hakuna bonasi au kizidishi kinachoweza kutumika katika kukokotoa ada zinazotolewa.
2. Ada haziwezi kutolewa na gharama zinazohusiana haziwezi kurejeshwa katika hatua au shauri lolote kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA kwa huduma zilizotolewa baada ya ofa ya maandishi ya malipo uliyopatiwa ikiwa:
    a. ofa hiyo inatolewa ndani ya muda uliowekwa na Kanuni ya 68 ya Kanuni za Serikali kuu za Uendeshaji wa Kesi za Madai au, iwapo shauri hilo au mapitio ya ngazi ya jimbo, wakati wowote zaidi ya siku 10 kabla ya kesi hiyo kuanza;
    b. ofa haikubaliki ndani ya siku 10; **na**
    c. mahakama imeona kwamba afueni uliyopata haikufai kuliko ofa ya kukubaliana.

   Licha ya vizuizi hivi, utoaji wa ada za mawakili na gharama zinazohusiana nayo unaweza kulipwa ikiwa utashinda na ulikuwa na sababu za kutosha za kukataa ombi la kulipa.
3. Ada haziwezi kutolewa kuhusiana na mkutano wowote wa timu ya Mpango wa Elimu Iliopambanuliwa (IEP) isipokuwa kama mkutano huo ufanyike kama matokeo ya shauri la kiutawala au hatua ya mahakama. Ada pia haiwezi kutolewa kwa upatanishi kama ilivyofafanuliwa katika kichwa cha habari ***Upatanishi.***

Mkutano wa usuluhishi, kama ilivyofafanuliwa katika kichwa cha habari ***mkutano wa Usuluhishi***, hauchukuliwi kama mkutano ulioitishwa kwa sababu ya shauri la utawala au hatua ya mahakama na pia halichukuliwi kama shauri la utawala au hatua ya mahakama kwa madhumuni ya utoaji wa ada hizi za mawakili.

Mahakama inapunguza, kadri inavyofaa, kiasi cha ada za mawakili zinazotolewa kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA, iwapo mahakama itaona kwamba:

1. Wewe au wakili wako, wakati wa hatua au shauri, ulichelewesha bila sababu utatuzi wa mwisho wa mzozo;
2. kiasi cha ada za mawakili zilizoidhinishwa kutolewa isivyofaa zinazidi bei ya saa iliyopo katika jamii kwa huduma zinazofanana kutoka kwa mawakili wenye ujuzi, sifa na uzoefu unaofanana;

3. muda uliotumika na huduma za kisheria zilizotolewa zilikuwa nyingi kwa kuzingatia hali ya kesi au mwenendo wa kesi; **na/au**
4. wakili anayekuwakilisha hakuipatia wilaya ya shule taarifa inayofaa katika notisi ya ombi la shauri kama ilivyobainishwa katika kichwa cha habari ***Malalamiko Yanayostahili***.

Hata hivyo, mahakama inaweza isipunguze ada ikiwa mahakama itabaini kuwa wilaya ya shule ilicheleweshà bila sababu za msingi suluhu ya mwisho ya hatua au shauri au kulikuwa na ukiukaji kwa mujibu wa masharti ya ulinzi wa haki za mtoto mwenye ulemavu na wazazi wake wa Sehemu B ya IDEA.

# Taratibu za Kuwaadhibu Watoto Wenye Ulemavu

## *Mamlaka ya Wafanyakazi wa Shule*

*34 C.F.R. § 300.530 na SBE Rule § 0520-01-09-.15*

**Uamuzi wa kesi kwa kesi**

Wafanyakazi wa shule wanaweza kuzingatia hali zozote za kipekee kwa msingi wa kesi baada ya nyingine wakati wa kubainisha kama mabadiliko ya mahali pa shule yaliyofanywa kwa mujibu wa masharti yafuatayo yanayohusiana na nidhamu yanafaa kwa mtoto mwenye ulemavu anayekiuka kanuni za shule za maadili ya mwanafunzi.

**Jumla**

Kiasi kwamba pia wanachukua hatua hizo kwa watoto wasio na ulemavu, wafanyakazi wa shule wanaweza, kwa muda usiozidi siku **10 za shule**, kumwondoa mtoto mwenye ulemavu ambaye anakiuka kanuni za maadili ya mwanafunzi kutoka kwenye darasa lake la sasa hadi kwenye mazingira mbadala yanayofaa ya elimu kwa muda (ambao lazima yaamuliwe na timu ya Mpango wa Elimu Iliopambanuliwa (IEP)), mazingira mengine, au kusimamishwa. Wafanyakazi wa shule wanaweza pia wanaweza kuongeza **siku zisizozidi 10 za shule** za kuondolewa kwa mwanafunzi katika mwaka huo huo wa shule kwa matukio tofauti ya utovu wa nidhamu ilimradi kuondolewa huko hakufanyi mabadiliko ya mahali (tazama ***Mabadiliko ya Mahali kwa Sababu ya Uondoaji wa Kinidhamu*** kwa ajili ya ufafanuzi).

Mara baada ya mtoto mwenye ulemavu kuondolewa kwenye nafasi yake ya sasa kwa jumla ya **siku 10 za shule** katika mwaka huo huo wa shule, wilaya ya shule lazima, wakati wa siku zozote zinazofuata za kuondolewa katika mwaka huo wa shule, kutoa huduma kwa kiwango kinachohitajika kama inavyoelezwa katika kichwa kidogo ***Huduma***.

**Mamlaka ya ziada**

Ikiwa tabia iliyokiuka kanuni za maadili ya mwanafunzi haikudhihirisha ulemavu wa mtoto (angalia ***Uamuzi wa Udhihirisho***) na mabadiliko ya kinidhamu ya sehemu yangezidi **siku 10 za shule** mfululizo, wafanyakazi wa shule wanaweza kutumia taratibu za kinidhamu kwa mtoto huyo aliye na ulemavu kwa namna ile ile na kwa muda sawa na vile ingekuwa kwa watoto wasio na ulemavu, isipokuwa shule lazima itoe huduma kwa mtoto huyo kama ilivyoelezwa katika kichwa cha habari ***Huduma***. Timu ya IEP ya mtoto huamua mpangilio mbadala wa muda wa elimu kwa huduma hizo.

**Huduma**
Huduma ambazo ni lazima zitolewe kwa mtoto mwenye ulemavu ambaye ameondolewa kwenye nafasi ya sasa ya mtoto zinaweza kutolewa katika mazingira mbadala ya muda ya elimu.

Wilaya ya shule inapaswa tu kutoa huduma kwa mtoto mwenye ulemavu ambaye ameondolewa kwenye nafasi yake ya sasa kwa **siku 10 za shule au chini ya hapo** katika mwaka huo wa shule ikiwa inatoa huduma kwa mtoto asiye na ulemavu ambaye ameondolewa vile vile.

Mtoto mwenye ulemavu ambaye ameondolewa mahali alipo kwa sasa kwa zaidi ya **siku 10 za shule** lazima:

1. aendelee kupokea huduma za elimu, ili kumwezesha mtoto kuendelea kushiriki katika mtaala wa elimu ya wote, ingawa katika mazingira mengine, na kuendelea kufikia malengo yaliyowekwa katika IEP ya mtoto; **na**
2. apokee, kadri inavyofaa, tathmini ya utendaji kazi na huduma za kushughulikia tabia na marekebisho ambayo yameundwa kushughulikia ukiukaji wa tabia ili usijirudie tena.

Baada ya mtoto mwenye ulemavu kuondolewa kwenye nafasi yake ya sasa kwa **siku 10 za shule** katika mwaka huo huo wa shule, na **ikiwa** kuondolewa kwa sasa ni **kwa siku 10 za shule** mfululizo au chini ya hapo **na ikiwa** kuondolewa huko sio mabadiliko ya upangaji sehemu (tazama ufafanuzi hapa chini), **kisha** wafanyakazi wa shule, kwa kushauriana na angalau mmoja wa walimu wa mtoto, huamua ni kwa kiwango gani huduma zinahitajika ili kumwezesha mtoto kuendelea kushiriki katika mtaala wa elimu ya wote, ingawa katika mazingira mengine, na maendeleo kuelekea kufikia malengo yaliyowekwa katika IEP ya mtoto.

Ikiwa kuondolewa huko ni mabadiliko ya upangaji (angalia ufafanuzi hapa chini), timu ya IEP ya mtoto huamua huduma zinazofaa ili kumwezesha mtoto kuendelea kushiriki katika mtaala wa elimu ya wote, ingawa katika mazingira mengine, na kuendelea kufikia malengo yaliyowekwa katika IEP ya mtoto.

**Uamuzi wa udhihirisho**
Ndani ya **siku 10 za shule** baada ya uamuzi wowote wa kubadilisha nafasi ya mtoto mwenye ulemavu kwa sababu ya ukiukaji wa kanuni za maadili ya mwanafunzi (isipokuwa kama kuondolewa huko ni kwa **siku 10 za shule** mfululizo au chini ya hapo na sio mabadiliko ya upangaji), wilaya ya shule, mzazi, na wahusika wa timu ya IEP (kama ilivyoamuliwa na mzazi na wilaya ya shule) lazima wapitie taarifa zote muhimu katika faili ya mwanafunzi, ikijumuisha IEP ya mtoto, uchunguzi wowote wa mwalimu, na taarifa yoyote muhimu iliyotolewa na wazazi kubaini:

1. ikiwa mwenendo unaozungumziwa ulisababishwa na, au ulikuwa na uhusiano wa moja kwa moja na mkubwa na, ulemavu wa mtoto; **au**
2. ikiwa mwenendo unaozungumziwa ulikuwa matokeo ya moja kwa moja ya wilaya ya shule kushindwa kutekeleza IEP ya mtoto.

Ikiwa wilaya ya shule, mzazi, na wahusika wa timu ya IEP ya mtoto watabaini kuwa mojawapo ya masharti hayo yalitimizwa, ni lazima mwenendo huo uamuliwe kuwa dhihirisho la ulemavu wa mtoto.

Iwapo wilaya ya shule, mzazi, na wahusika wa timu ya IEP ya mtoto watabaini kuwa mwenendo unaozungumziwa ulikuwa matokeo ya moja kwa moja ya wilaya ya shule kushindwa kutekeleza IEP, wilaya ya shule lazima ichukue hatua za haraka kurekebisha kasoro hizo.

**Uamuzi kwamba tabia hiyo ilikuwa dhihirisho la ulemavu wa mtoto**
Ikiwa wilaya ya shule, mzazi, na wahusika wa timu ya IEP watabaini kuwa mwenendo huo ulikuwa dhihirisho la ulemavu wa mtoto, timu ya IEP lazima:

1. ifanye tathmini ya tabia ya utendaji, isipokuwa kama wilaya ya shule imefanya tathmini ya tabia ya utendaji kabla ya tabia ambayo ilisababisha mabadiliko ya upangaji kutokea, na kutekeleza mpango wa kushughulikia tabia kwa mtoto; **au**
2. ikiwa mpango wa kushughulikia tabia tayari umeandaliwa, pitia mpango wa kushughulikia tabia, na uurekebishe inapohitajika kushughulikia tabia.

Isipokuwa kama ilivyoelezwa katika ***hali Maalum***, wilaya ya shule lazima imrudishe mtoto mahali ambapo aliondolewa, isipokuwa kama mzazi na wilaya wamekubaliana na mabadiliko ya mahali kama sehemu ya marekebisho ya mpango wa kushughulikia tabia.

**Mazingira maalum**
Iwe tabia hiyo ilikuwa dhihirisho la ulemavu wa mtoto au la, wafanyakazi wa shule wanaweza kumwondoa mwanafunzi kwenye mazingira mbadala ya muda ya elimu (yaliyoamuliwa na timu ya mtoto ya IEP) kwa hadi siku 45 za shule ikiwa mtoto:

1. hubeba silaha (tazama ufafanuzi hapa chini) kwenda nayo shuleni au huwa na silaha shuleni, kwenye eneo la shule, au katika hafla ya shule iliyo chini ya mamlaka ya Idara ya Elimu ya Tennessee au wilaya ya shule;
2. kwa kujua huwa na au hutumia dawa za kulevya (angalia ***sehemu*** ya Ufafanuzi) au huuza au anashawishi uuzaji wa dawa za kulevya (tazama ***sehemu*** ya Ufafanuzi) akiwa shuleni, kwenye eneo la shule, au katika shughuli za shule iliyo chini ya mamlaka ya Idara ya Elimu ya Tennessee au wilaya ya shule; **au**
3. amesababisha jeraha kubwa la mwili (angalia ***sehemu ya Ufafanuzi***) kwa mtu mwingine akiwa shuleni, kwenye eneo la shule, au katika hafla ya shule iliyo chini ya mamlaka ya Idara ya Elimu ya Tennessee au wilaya ya shule.

## Fasili

*Madawa ya kulevya* inamaanisha dawa au vitu vingine vilivyobainishwa katika jedwali la I, II, III, IV, au V katika kifungu cha 202(c) cha Sheria ya Dawa za Kulevya (21 U.S.C. 812(c)).

*Dawa haramu* maana yake ni dawa zinazozibitiwa, lakini haijumuishi dawa zinazodhibitiwa ambazo zinamilikiwa kisheria au zinazotumiwa chini ya usimamizi wa mtaalamu wa afya aliyeidhinishwa au ambacho kinamilikiwa kisheria au kinatumiwa chini ya mamlaka nyingine yoyote kwa mujibu wa IDEA au kwa mujibu wa sheria nyingine yoyote ya serikali kuu.

*Jeraha kubwa la mwili* lina maana inayotolewa na neno ''jeraha kubwa la mwili'' kwa mujibu wa aya ya (3) ya kifungu kidogo cha (h) cha kifungu cha 1365 cha sura ya 18, Kanuni ya Sheria ya Marekani.

*Silaha* ina maana inayotolewa na neno ''silaha hatari'' kwa mujibu wa aya ya (2) ya kifungu kidogo cha (g) cha kifungu cha 930 cha sura ya 18, Kanuni ya Sheria ya Marekani.

### Taarifa

Katika tarehe ambayo wilaya ya shule inafanya uamuzi wa kumwondoa mtoto ambayo ni mabadiliko ya kumpangia darasa mtoto kwa sababu ya ukiukaji wa kanuni za maadili ya mwanafunzi, wilaya ya shule lazima iwajulishe wazazi kuhusu uamuzi huo na kuwapa wazazi taarifa ya ulinzi wa haki za mtoto mwenye ulemavu na wazazi wake.

## *Mabadiliko ya Darasa kwa Sababu za Kinidhamu*

*34 C.F.R. § 300.536*

Kuondolewa kwa mtoto mwenye ulemavu kutoka kwenye nafasi ya sasa ya elimu ya mtoto ni **mabadiliko ya upangaji** ikiwa:

1. Kuondolewa huko ni kwa zaidi ya siku 10 za shule mfululizo; **au**
2. Mtoto amekabiliwa na msururu wa kuondolewa ambako kunafanya kuwa mazoea sababu:
    a. mfululizo wa kuondolewa kunafanya jumla ya zaidi ya siku 10 za shule katika mwaka wa shule;
    b. tabia ya mtoto inafanana kwa kiasi kikubwa na tabia ya mtoto katika matukio ya awali ambayo yalisababisha mfululizo wa kuondolewa; **na**
    c. ya mambo ya ziada kama vile urefu wa kila kuondolewa, jumla ya muda ambao mtoto ameondolewa, na ukaribu wa kuondolewa kwa kila mmoja.

Ikiwa mtindo wa uondoaji uliosababisha mabadiliko ya upangaji unaamuliwa kwa msingi wa jambo moja baada ya jingine na wilaya ya shule na, ikiwa itapingwa, inaweza kupitiwa kwa kutumia mchakato unaostahili na taratibu za kimahakama.

## *Uamuzi wa Mazingira*

*34 C.F.R. § 300.531*

Timu ya Mpango wa Elimu Iliopambanuliwa (IEP) lazima iamue mazingira mbadala wa muda wa elimu kwa kuondolewa ambako ni **mabadiliko ya upangaji** na uondoaji ambao upo katika vichwa vidogo vya habari ***Mamlaka ya Ziada*** na ***Mazingira Maalum***.

## *Rufaa*

*34 C.F.R. § 300.532*

### Jumla

Mzazi wa mtoto mwenye ulemavu anaweza kuwasilisha malalamiko ili kuomba shauri lisikilizwe ikiwa hakubaliani na:

1. uamuzi wowote kuhusu upangaji uliofanywa chini ya masharti haya ya nidhamu; **au**
2. uamuzi wa udhihirisho (tazama ***sehemu ya uamuzi wa Udhihirisho***).

Wilaya ya shule inaweza kuwasilisha malalamiko ili kuomba shauri lisikilizwe ikiwa inaamini kwamba kuendelea na darasa la sasa kwa mtoto kuna uwezekano mkubwa wa kusababisha jeraha kwa mtoto au kwa wengine.

**Mamlaka ya hakimu kiongozi**
JHakimu kiongozi anayekidhi vigezo vilivyofafanuliwa katika kichwa kidogo cha habari cha ***Hakimu kiongozi*** lazima aendeshe usikilizwaji wa mashauri na kufanya uamuzi. Hakimu kiongozi anaweza:

1. kumrejesha mtoto mwenye ulemavu katika nafasi ambayo aliondolewa ikiwa hakimu kiongozi ataona kuwa kuondolewa kwake ni ukiukaji wa mahitaji yaliyoelezwa katika kichwa cha habari cha ***Mamlaka ya Wafanyakazi wa Shule*** au kwamba tabia ya mtoto ilikuwa dhihirisho la ulemavu wa mtoto; **au**
2. kuamuru mabadiliko ya upangaji wa mtoto mwenye ulemavu kwenye mazingira mbadala ya muda ya elimu yanaofaa kwa muda usiozidi siku 45 za shule ikiwa hakimu kiongozi ataona kwamba kuendelea kuwa katika sehemu ya sasa ya mtoto kuna uwezekano mkubwa wa kusababisha jeraha kwa mtoto huyo au kwa wengine.

Taratibu hizi za usikilizaji wa shauri zinaweza kurudiwa ikiwa wilaya ya shule inaamini kwamba kumrejesha mtoto katika eneo la awali kuna uwezekano mkubwa wa kusababisha jeraha kwa mtoto huyo au kwa wengine.

Wakati wowote mzazi au wilaya ya shule inapowasilisha shauri la malalamiko kuomba usikilizaji huo, shauri hilo lazima lisikilizwe kama linakidhi masharti yaliyofafanuliwa katika kichwa cha habari cha ***Taratibu za Malalamiko, Usikilizaji wa Malalamiko Yanayostahili***, isipokuwa kama ifuatavyo:

1. Wilaya ya shule lazima ipange haraka mchakato wa usikilizaji shauri, ambao lazima ufanyike ndani ya siku **20** za shule tangu tarehe ya usikilizwaji wa shauri ilipoombwa na lazima utoe uamuzi ndani ya siku **10** za shule baada ya kusikilizwa.
2. Isipokuwa kama wazazi na wilaya ya shule watakubaliana kwa maandishi kuacha mkutano, au wakubali kutumia upatanishi, mkutano wa usuluhishi lazima ufanyike ndani ya siku **saba (7)** baada ya kupokea taarifa ya malalamiko hayo. Usikilizwaji wa shauri unaweza kuendelea isipokuwa kama suala limetatuliwa kwa kuridhisha pande zote mbili ndani ya siku **15** baada ya kupokea malalamiko hayo.

Mhusika anaweza kukata rufaa dhidi ya uamuzi huo katika hatua ya usikilizaji wa shauri wa haraka kwa njia sawa na wanavyoweza kutoa maamuzi katika mashauri mengine (angalia sehemu ya ***Rufaa***).

## *Kupangwa Darasa Wakati wa Rufaa*

*34 C.F.R. § 300.533*

Pale, kama ilivyoelezwa hapo juu, mzazi au wilaya ya shule inapowasilisha malalamiko kuhusiana na masuala ya kinidhamu, mtoto lazima (isipokuwa kama mzazi na wilaya ya shule wamekubaliana vinginevyo) abaki katika mazingira mbadala ya muda ya elimu akisubiri uamuzi hakimu kiongozi au hadi kumalizika kwa muda wa kuondolewa kama ilivyoainishwa na kuelezwa katika kichwa cha habari ***Mamlaka ya Wafanyakazi wa Shule***, chochote kitakachotokea kwanza.

## *Ulinzi kwa Watoto Ambao Bado Hawastahiki Kupata Elimu Maalum na Huduma Zinazohusiana Nayo*

*34 C.F.R. § 300.534*

### Jumla

Ikiwa mtoto hajatambuliwa kuwa anastahili kupata elimu maalum na huduma zinazohusiana nayo na anakiuka kanuni za nidhamu za wanafunzi, lakini wilaya ya shule ilikuwa inafahamu (kama ilivyobainishwa hapa chini) kabla ya tabia iliyosababisha hatua ya kinidhamu kuchukuliwa, kwamba mtoto huyo alikuwa mtoto mwenye ulemavu, basi mtoto anaweza kudai ulinzi wowote ulioelezwa katika taarifa hii.

#### Msingi wa maarifa kwa maswala ya kinidhamu

Wilaya ya shule lazima ichukuliwe kuwa na ufahamu kuwa mtoto ni mtoto mwenye ulemavu ikiwa, kabla ya tabia iliyosababisha hatua ya kinidhamu kutokea:

1. mzazi wa mtoto alionyesha wasiwasi wake kwa maandishi kwamba mtoto anahitaji elimu maalum na huduma zinazohusiana nayo na usimamizi au wafanyakazi wa utawala wa shirika stahiki la elimu au mwalimu wa mtoto;
2. mzazi aliomba tathmini inayohusiana na ustahiki wa elimu maalum na huduma zinazohusiana nayo kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA; **au**
3. mwalimu wa mtoto au wafanyakazi wengine wa wilaya ya shule walionyesha tatizo mahususi kuhusu mtindo wa tabia ulioonyeshwa na mtoto moja kwa moja kwa mkurugenzi wa elimu maalum wa wilaya ya shule au kwa wasimamizi wengine wa wilaya ya shule.

### Isipokuwa

Wilaya ya shule haitachukuliwa kuwa na ujuzi huo ikiwa:

1. mzazi wa mtoto hajaruhusu tathmini ya mtoto au alikataa huduma za elimu maalum; **au**
2. mtoto ametathminiwa na kubainika kuwa si mtoto mwenye ulemavu kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA.

#### Masharti yanayotumika ikiwa hakuna msingi wa maarifa

Iwapo kabla ya kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya mtoto, wilaya ya shule haina ufahamu kwamba mtoto huyo ni mtoto mwenye ulemavu, kama ilivyoelezwa hapo juu katika vichwa vidogo vya habari, ***Msingi wa ujuzi wa masuala ya kinidhamu*** na ***Isipokuwa***, mtoto huyo anaweza kuchukuliwa hatua za kinidhamu zinazotumika kwa watoto wasio na ulemavu wanaojihusisha na tabia zinazolingana na hizo.

Hata hivyo, ikiwa ombi limetolewa kwa ajili ya tathmini ya mtoto katika kipindi ambacho mtoto anachukuliwa hatua za kinidhamu, tathmini lazima ifanyike kwa njia ya haraka.

Hadi tathmini inapokuwa imekamilika, mtoto huyo atabaki katika nafasi ya elimu iliyoamuliwa na mamlaka ya shule, ambayo inaweza kujumuisha kusimamishwa au kufukuzwa bila kupewa huduma za elimu.

Iwapo mtoto huyo amebainika kuwa mtoto mwenye ulemavu, kwa kuzingatia taarifa kutoka kwenye tathmini iliyofanywa na wilaya ya shule na taarifa iliyotolewa na wazazi, wilaya ya shule

lazima itoe elimu maalum na huduma zinazohusiana nayo kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA, ikiwemo mahitaji ya kinidhamu yaliyoelezwa hapo awali.

### *Rufaa na Hatua za Chombo cha Utekelezaji wa Sheria na Mamlaka za Mahakama*

*34 C.F.R. § 300.535*

Sehemu B ya IDEA:

1. haiikatazi shirika kuripoti uhalifu uliofanywa na mtoto mwenye ulemavu kwa mamlaka husika; **au**
2. haiwazuii watekelezaji sheria wa jimbo na mamlaka za mahakama kutekeleza majukumu yao kuhusu matumizi ya sheria ya serikali kuu na jimbo kwa uhalifu uliotendwa na mtoto mwenye ulemavu.

**Utumaji wa kumbukumbu**

Ikiwa wilaya ya shule itaripoti uhalifu uliotendwa na mtoto mwenye ulemavu, wilaya ya shule:

1. lazima ihakikishe kwamba nakala za elimu maalum na taarifa za nidhamu ya mtoto zinatumwa kwa ajili ya uamuzi wa mamlaka ambazo shirika limeripoti uhalifu kwao;

   **na**
2. inaweza kutuma nakala za taarifa za elimu maalum na za nidhamu za mtoto kadri inavyoruhusiwa na Sheria ya Haki za Kielimu na Faragha ya Familia (FERPA).

## Masharti ya Upangaji wa Upande Mmoja Unaofanywa na Wazazi wa Watoto katika Shule Binafsi kwa Gharama za Serikali

### *Jumla*

*34 C.F.R. § 300.148*

Sehemu B ya IDEA haihitaji wilaya ya shule kulipia gharama ya elimu, ikiwa ni pamoja na elimu maalum na huduma zinazohusiana nayo, za mtoto wako mwenye ulemavu katika shule au kituo binafsi ikiwa wilaya ya shule ilihakikisha Elimu ya Umma Inayofaa Bila Malipo (FAPE) inapatikana kwa mtoto wako na umeamua kumpeleka mtoto huyo katika shule au kituo binafsi. Hata hivyo, wilaya ya shule ambako shule binafsi iko lazima imjumuishe mtoto wako katika idadi ya watu ambao mahitaji yao yanashughulikiwa kwa mujibu wa masharti ya Sehemu ya B kuhusu watoto ambao wamepelekwa na wazazi wao katika shule binafsi kwa mujibu wa 34 C.F.R. §§ 300.131 hadi 300.144.

**Urejeshaji wa gharama kwa uandikishaji wa shule binafsi**

Iwapo mtoto wako alipata elimu maalum na huduma zinazohusiana nayo hapo awali chini ya mamlaka ya wilaya ya shule na unaamua kumwandikisha mtoto wako katika shule binafsi ya chekechea, shule ya msingi au sekondari bila idhini au kupelekwa na wilaya ya shule, mahakama au hakimu kiongozi anaweza kulitaka shirika kukurejeshea gharama ya uandikishaji huo ikiwa mahakama au hakimu kiongozi ataona kuwa shirika halikutoa Elimu ya Umma Inayofaa (FAPE) kwa mtoto wako kwa wakati ufaao kabla ya uandikishaji huo na kwamba uandikishaji wa shule binafsi unafaa. Jaji kiongozi au mahakama inaweza kuona uandikishaji wako kuwa mwafaka, hata kama shule au kituo hicho hakifikii viwango vya serikali vinavyotumika kwa elimu inayotolewa na wilaya za shule.

**Ukomo wa kurejeshewa gharama**

Gharama ya kurejeshwa iliyofafanuliwa katika aya ya hapo juu inaweza kupunguzwa au kukataliwa katika hali zifuatazo:

1. Iwapo: (a) katika mkutano wa hivi karibuni wa Mpango wa Elimu Iliopambanuliwa (IEP) uliohudhuria kabla ya kuondolewa kwa mtoto wako katika shule ya serikali, hukutoa taarifa kwenye timu ya IEP kwamba unakataa upangaji uliopendekezwa na wilaya ya shule ili kumpatia FAPE mtoto wako, kiwemo kueleza wasiwasi wako na nia yako ya kumwandikisha mtoto wako katika shule binafsi kwa gharama ya serikali; au (b) angalau siku 10 za kazi (pamoja na sikukuu yoyote ambayo hutokea siku ya kazi) kabla ya kuondolewa kwa mtoto wako katika shule ya serikali, hukutoa notisi ya maandishi kwa wilaya ya shule kuhusu taarifa hiyo.
2. Iwapo, kabla ya kumwondoa mtoto wako katika shule ya serikali, wilaya ya shule ilikupa taarifa ya maandishi mapema kuhusu nia yake ya kumtathmini mtoto wako (pamoja na taarifa ya madhumuni ya tathmini ambayo ilikuwa sahihi na ya kuridhisha), lakini hukuhakikisha mtoto huyo anapatikana kwa ajili ya tathmini.
3. Ikiwa mahakama inaona kuwa matendo yako hayakuwa ya busara.

Hata hivyo, gharama ya kurejeshwa:

1. haipaswi kupunguzwa au kukataliwa kwa kushindwa kutoa notisi ikiwa: (a) shule ilikuzuia kutoa notisi; (b) ulikuwa haujapokea notisi ya wajibu wako wa kutoa notisi iliyoelezwa hapo juu; au (c) kutii masharti ya hapo juu kunaweza kusababisha madhara ya kimwili kwa mtoto wako; **na**
2. inaweza, kwa uamuzi wa mahakama au hakimu kiongozi, isipunguzwe au kukataliwa kwa kushindwa kwa wazazi kutoa notisi inayohitajika ikiwa: (a) mzazi hajui kusoma na kuandika au hawezi kuandika kwa Kiingereza; au (b) kutii masharti ya hapo juu kunaweza kusababisha madhara makubwa ya kihisia kwa mtoto.

# Tennessee Department of Education
# Special Education Administrative Complaint Form

Office of General Counsel
Andrew Johnson Tower, 9th Floor
710 James Robertson Parkway
Nashville, Tennessee 37243
**Barua pepe kwenda wilaya ya shule na dispute.resolution@tn.gov**

| **Jina la Mlalamikaji** [1] | Uhusiano kwa Mtoto | Barua pepe ya Mlalamikaji |
|---|---|---|

| **Anwani** ***Mtaa, Jiji, Jimbo, Msimbo wa Posta*** | Namba ya Simu (*Msimbo/Namba ya Eneo*)<br>Nyumbani<br>Kazini<br>Simu ya Mkononi |
|---|---|

| **Jina la Mtoto** | Tarehe ya Kuzaliwa ya Mtoto (*Mwezi/Siku/Mwaka*) | Ulemavu wa Mtoto |
|---|---|---|

| **Anwani ya Mtoto (kama ni tofauti na ya Mlalamikaji) (*Mtaa, Jiji, Jimbo, Msimbo wa Posta*) mawasiliano** | ***Kwa watoto wasio na makazi toa taarifa ya** |
|---|---|

| Mfumo wa Shule | Shule Anayosoma Mtoto |
|---|---|

Tafadhali weka alama kwenye uvunjifu unaoshukiwa wa kanuni za elimu maalum. Hati za madai ya ukiukaji lazima zitolewe kwa kila kisanduku kilichowekwa alama:

- ☐ Kushindwa kutathmini/kubainisha elimu maalum na huduma zinazohusiana nayo
- ☐ Kushindwa kufuata taratibu za timu za Mpango wa Elimu Iliopambanuliwa (IEP)
- ☐ Kushindwa kutekeleza marekebisho ya IEP
- ☐ Kushindwa kutekeleza huduma za IEP
- ☐ Kushindwa kutoa IEP inayofaa ili kukidhi mahitaji ya mwanafunzi
- ☐ Kushindwa kufuata taratibu sahihi za kusimamishwa/kufukuzwa kwa mwanafunzi aliyetambuliwa kuwa
- ☐ na ulemavu Kushindwa kutoa fursa ya kupitia/kukagua taarifa za elimu
- ☐ Kushindwa kuzingatia ombi la tathmini huru ya elimu (IEE) Kushindwa kufanya
- ☐ upya tathmini ya kina
- ☐ Kushindwa kumruhusu mzazi kushiriki katika maamuzi ya elimu
- ☐ Walimzuia mwanafunzi wangu isivyofaa
- ☐ Walimtenga mwanafunzi wangu isivyofaa
- ☐ Nyingine) ____________________________________________

[1] *Ikiwa mtu anayewasilisha malalamiko si mzazi wa mtoto, malalamiko haya lazima yajumuishe idhini ya Idara ya Elimu ya Tennessee (TDOE) ili kutoa taarifa. Tafadhali wasiliana na TDOE kupata nakala ya fomu ya idhini.*

**Toa maelezo ya tatizo, ikiwemo ukweli** na tarehe zinazohusiana na madai yote yaliyowekwa alama kwenye ukurasa wa 1. Malalamiko lazima yadai ukiukaji ambao ulifanyika si zaidi ya mwaka mmoja kabla ya tarehe ambayo malalamiko haya yanapokelewa na Idara ya Elimu ya Tennessee (TDOE). Jumuisha hati zinazotetea madai yako kama kiambatisho cha fomu hii. TDOE itatupilia mbali madai, au ikiwezekana, malalamiko hayo kwa ujumla wake, wakati madai hayo, kwa muonekano wake au kama yalivyofafanuliwa, inaposhindwa kudai ukiukaji wa sheria ya elimu maalum. Iwapo rekodi ya sauti au video yenye tarehe itawasilishwa, lazima kuwe na marejeleo kuhusu muda ndani ya rekodi ambayo maelezo ya msaada yanapatikana:

## Fomu ya Malalamiko ya Utawala ya Idara ya Elimu Maalum ya Tennessee Ukurasa wa: 3

| |
|---|
| Orodhesha watu wowote, kama wapo, ambao tayari umewasiliana nao kutatua malalamiko haya, pamoja na majibu yao ya ombi lako: |
| **Toa mapendekezo ya utatuzi wa tatizo kwa kiwango kinachojulikana na kinachopatikana.** [2] |
| Kwa kutia sahihi hapa chini, unadai kuwa ungependa TDOE ichunguze malalamiko na kukuarifu kuhusu matokeo yake. Unaelewa kwamba unaweza kuombwa kutoa hati za ziada. Pia unaelewa kwamba TDOE ina siku sitini (60) baada ya kupokea malalamiko, ili kukamilisha uchunguzi. |

| **Sahihi ya Mlalamikaji (*Sehemu nzito inahitajika;* *wengine ni msaada*)** | **Tarehe Iliyosainiwa (*Mwezi/Siku/Mwaka)*** |
|---|---|
| | |

[2] **UPATANISHI** unatolewa bure kwa wazazi na wafanyakazi wa shule. Upatanishi unahimizwa na unaweza kuwa muhimu kwenye suala lako. Hata hivyo, tafadhali fahamu kwamba upatanishi ni mfumo wa hiari wa kutatua mizozo. Pande zote mbili lazima zikubali kusuluhisha masuala yao kabla ya kuanza kwa mchakato wa upatanishi. Bofya HAPA kupata taarifa za ziada kuhusu upatanishi.

*Suluhu iliyopendekezwa inalenga kwa upande fulani kumsaidia mlalamikaji na LEA katika kufikia suluhu ya mapema ya malalamiko. Hatua yoyote ya ukarabati ambayo inaweza kuhitajika kuhusiana na malalamiko hayo iko ndani ya uamuzi wa TDOE. Mapendekezo fulani ya hatua za kuchukuliwa, kama vile nidhamu au kusimamishwa kazi kwa wafanyikazi wa shule, hayako chini ya mamlaka ya TDOE.*

*Taarifa Zinazohitajika: A* ***uga wa ujasiri*** *kwenye fomu ya malalamiko ya mfano inaonyesha habari zinazohitajika. Fomu za malalamiko lazima zijumuishe taarifa kwamba shirika la umma limekiuka matakwa ya sheria maalum ya elimu; ukweli ambao taarifa hiyo inategemea; saini na taarifa ya mawasiliano kwa mlalamikaji; kama madai ya ukiukwaji kwa heshima ya mtoto maalum - jina na anwani ya mtoto, jina la shule mtoto anahudhuria, maelezo ya asili ya tatizo, ikiwa ni pamoja na ukweli kuhusiana na tatizo, na mapendekezo ya utatuzi wa tatizo. Ikiwa malalamiko yanawasilishwa kwa niaba ya mtoto asiye na makazi, toa maelezo ya mawasiliano kwa mtoto na jina la shule ambayo mtoto anahudhuria. Malalamiko ya kumbuka lazima yadai ukiukaji ambao ulitokea si zaidi ya mwaka mmoja kabla ya tarehe ambayo malalamiko yanawasilishwa. Chama kinachowasilisha malalamiko lazima kipeleke nakala ya malalamiko kwa shirika la umma linalomhudumia mtoto wakati huo chama kinawasilisha malalamiko kwa serikali.*

# Tennessee Department of Education

## Special Education Mediation Request Form

Office of General Counsel
Andrew Johnson Tower, 9th Floor
710 James Robertson Parkway
Nashville, Tennessee 37243

**Barua pepe kwenda wilaya ya shule na dispute.resolution@tn.gov**

| Jina la Mtoto | Tarehe ya Kuzaliwa ya Mtoto *Mwezi/Siku/Mwaka* | Ulemavu wa Mtoto |
|---|---|---|
| Mfumo wa Shule<br>Alamo City Schools | Shule Anayosoma Mtoto | |

| Taarifa za Mzazi/Mlezi | | Taarifa za Kiongozi wa Shirika la Elimu la Serikali ya Mtaa (LEA) | |
|---|---|---|---|
| Jina | | Jina | |
| Anwani | | Anwani | |
| Jiji | Msimbo wa Posta | Jiji | Msimbo wa Posta |
| Simu ya Nyumbani | Simu ya Mkononi | Simu | Faksi |
| Anwani ya Barua pepe | | Anwani ya Barua pepe | |
| Kama umewakilishwa na mwana wakili | | Kama umewakilishwa na mwana wakili | |
| Jina la Wakili | | Jina la Wakili | |
| Anwani | | Anwani | |
| Jiji | Msimbo wa Posta | Jiji | Msimbo wa Posta |
| Simu | Faksi | Simu | Faksi |
| Anwani ya Barua pepe | | Anwani ya Barua pepe | |

Tunaelewa kwamba ombi hili ni la upatanishi pekee. Usikilizaji wa shauri ***haujaombwa***.

Tunaelewa kuwa ombi hili ni kwa ajili ya upatanishi sambamba na ombi la usikilizaji wa shauri linalostahili. Ombi la maandishi la usikilizwaji wa shauri linalostahili limetumwa kwa Mkurugenzi wa Shule.

Muhtasari wa masuala ambayo yatapatanishwa:

| Sahihi ya Mzazi/Mlezi | Tarehe | Sahihi ya Kiongozi wa LEA | Tarehe |
|---|---|---|---|
| | | | |

# Tennessee Department of Education

## Special Education Due Process Hearing Request Form

Office of General Counsel
Andrew Johnson Tower, 9th Floor
710 James Robertson Parkway
Nashville, Tennessee 37243

**Barua pepe kwenda wilaya ya shule na dispute.resolution@tn.gov**

| Taarifa ya Mzazi/Mtoto (Ijazwe na mzazi/mlezi na iwasilishwe LEA kwa ajili ya kushughulikiwa) | | |
|---|---|---|
| **Jina la Mtoto** | Tarehe ya Kuzaliwa ya Mtoto *Mwezi/Siku/Mwaka* | Ulemavu wa Mtoto |
| Jina la Mzazi/Mlezi | **Anwani ya Mtoto**/Mzazi/Mlezi *Mtaa, Jiji, Jimbo, Msimbo wa Posta* | |
| Simu | Anwani ya Barua pepe | Anwani Mzazi/Mlezi Mtaa, Jiji, Jimbo, Msimbo wa Posta |
| Wakili wa Mtoto/Mzazi/Mlezi | Anwani ya Wakili *Mtaa, Jiji, Jimbo, Msimbo wa Posta* | |
| Simu | Faksi | Anwani ya Barua pepe |
| Ombi la Usikilizwaji wa Shauri Linalostahili limeanzishwa na:<br>Mzazi/Mlezi    LEA (LEA itampatia mzazi taarifa anapowasilisha shauri) | | Shauri linapaswa kuwa:<br>Wazi    Faragha |
| Jina la Shule | | Jina la Wilaya ya Shule |

**Toa maelezo kamili ya asili ya tatizo na ukweli linalohusiana na utambulisho, tathmini, uandikishaji wa elimu (mabadiliko ya awali au yanayopendekezwa) au utoaji wa Elimu ya Umma Inayofaa Bila Malipo (FAPE).**

**Tafadhali toa suluhisho lililopendekezwa kwenye tatizo kwa kiwango kinachojulikana na kinachopatikana.**

| Taarifa Shirika la Elimu la Serikali ya Mtaa (LEA) (Ijazwe na wilaya ya shule) | | |
|---|---|---|
| Kiongozi wa LEA/Elimu Maalum | | Anwani ya LEA *Mtaa, Jiji, Jimbo, Msimbo wa Posta* |
| Simu | Faksi | Anwani ya Barua pepe |
| Shule Anayosoma/Aliyosoma Mtoto | | Ulemavu wa Mtoto |
| Wakili wa LEA | Anwani ya Wakili *Mtaa, Jiji, Jimbo, Msimbo wa Posta* | |
| Simu | Faksi | Anwani ya barua pepe |
| Tarehe Ombi limepokelewa na LEA | | Mahali Pa kusikilizia Shauri |

# Huduma za Utetezi

Kuna mashirika na taasis nyingi ambazo hutoa msaada, taarifa, mafunzo, na usaidizi katika kutetea watu wenye ulemavu katika jimbo la Tennessee. Zifuatazo ni miongoni mwa taasis chache ambazohutoa huduma bila malipo. Orodha ya kina ya taasis za huduma inaweza kupatikana kupitia Tennessee Disability Pathfinder (https://www.tnpathfinder.org/).

| | |
|---|---|
| ***Haki za Watu Wenye Ulemavu Tennessee*** ***(Disability Rights in Tennessee)*** (800) 342-1660 Barua pepe: GetHelp@disabilityrightstn.org | ***Sauti ya Tennessee ya Watoto*** ***(Tennessee Voices for Children)*** (800) 670-9882 Barua pepe: info@tnvoices.org |
| | |
| ***Msaada na Mafunzo kwa Wazazi wa Watoto Wenye mahitaji Maalum*** ***(Support and Training for Exceptional Parents) (STEP)*** (800) 280-7837 (Kiingereza) (800) 975-2919 (Kihispaniola) Barua pepe: gethelp@tnstep.info | ***Kizingo chs Tennesee*** ***(The Arc of Tennessee)*** (800) 835-7077 Barua pepe: info@thearctn.org |

# Huduma za Sheria za Bule na za Gharama Nafuu

Ifuatayo ni orodha ya ofisi zinazotoa huduma za kisheria bila malipo au za gharama nafuu ili kuwasaidia watu wenye ulemavu.

| | |
|---|---|
| ***Haki za Watu Wenye Ulemavu Tennessee*** ***(Disability Rights in Tennessee)*** (800) 342-1660 Tovuti: www.disabilityrightstn.org | ***Kliniki ya Sheria ya Vanderbilt*** ***(Vanderbilt Legal Clinic)*** (615) 322-4964 |
| | |
| ***Msaada wa Kisheria Tennessee Mashariki*** ***(Legal Aid of East Tennessee)*** (800) 238-1443 Website: www.laet.org | ***Huduma za Kisheria Tennessee Magharibi*** ***(West Tennessee Legal Services)*** (800) 372-8346 Tovuti: www.wtls.org |
| | |
| ***Jumuiya ya Msaada wa kisheria ya Tennessee ya Kati na Cumberlands*** ***(Legal Aid Society of Middle Tennessee and the Cumberlands)*** (800) 238-1443 Tovuti: www.las.org | |

Taarifa hii hutolewa kama huduma kwa watu wanaotafuta njia za ziada za msaada na taarifa. Idara haimaanishi kuwa huu ni uidhinishaji au pendekezo la mtu, shirika au huduma yoyote inayowakilishwa kwenye ukurasa huu.